# AMBOLA

## SEASON 02

### PALE MASHUJAA WANAPOLISALITI TAIFA LAO

# MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA

KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

HADITHI HII NI YA KUBUNI HAINA MAHUSIANO NA TUKIO LOLOTE LA KWELI.

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

**SIMULIZI ZA MAPENZI**

1.MISS TANZANIA
2.SERENA
3.BEFORE I DIE
4.BEYOND PAIN

**SIMULIZI ZA UPELELEZI**

5.PENIELA
6.QUEEN MONICA
7.THE FOOTBALL
8.I DIED TO SAVE PRESIDENT
9.KIAPO CHA JASUSI
10.KIKOSI CHA SIRI
11.SIRI
12.SCANDAL(KASHFA)
13.CAPTURE OR KILL MISSION
14.JAMII YA SIRI

**MAWASILIANO**

**0764294499**

© 2020 Masimulizi.Haki zote zimehifadhiwa

## ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

"Makubaliano yangu nanyi yalikuwa kumuondoa mtu mmoja .." alisema Gosu Gosu na mara alihisi kuguswa na kitu cha baridi kichwani.Alikuwa amewekewa bastola .

"Utafanya kazi au nikufumue kichwa chako sasa hivi? Aliuliza Jombaa ambaye sura yake ilionesha ukatili mkubwa

"Easy bro.....tufanye kazi" alisema Gosu Gosu akiielekeza bunduki katika ile meza yenye watu watatu wanaotakiwa

kuuawa.Kupitia lensi yenye nguvu iliyokuwa juu ya bunduki ile kubwa ya udunguaji aliona kitu kilichomshtua mno.

“Oh my God ! alisema Gosu Gosu kwa sauti ndogo

“Mathew Mulumbi.Anafanya nini pale? Halafu yule mwanamke mbona ni Regina.” Aliwaza Gosu Gosu.Alihisi kutetemeka mikono.

“Uko tayari? Aliuliza Jombaa lakini Gosu Gosu hakujibu kitu

“Uko tayari? Aliuliza tena Jombaa lakini bado Gosu Gosu

alikuwa kimya.Jombaa alimsogelea  Gosu Gosu.

“Kuna tatizo? Aliuliza

“Hakuna tatizo” alijibu Gosu Gosu

“Nitahesabu hadi tatu kisha utamaliza mchezo.Tunatakiwa kuondoka hapa haraka sana” alisema Jombba.Gosu Gosu aliwashuhudia wale jamaa waliowakuta mle chumbani wakizifunga kompyuta zao tayari kwa kuondoka.

“Moja ! alisema Jombaa

“Siwezi kumuua Mathew Mulumbi wala Regina.Lazima nitafute namna ya kufanya kuwaokoa” aliwaza Gosu Gosu

“Mb.....” alihesabu Jombaa lakini Gosu Gosu hakusubiri Jombaa amalize kuhesabu, aliachia risasi ya kwanza iliyompata Amani shingoni.Kabla hawajakaa sawa aliachia risasi ya pili iliyompata kichwani akaangukia mezani

Kitendo cha Amani kuanguka juu ya meza huku akivuja damu,kiliwashtua sana akina Mathew.Wakiwa bado wanashangaa, ilipigwa risasi ya tatu ambayo ilizisambaratisha chupa zilizokuwa mezani.Kama kima Mathew Mulumbi alimrukia Regina akamuangusha

chini.Alichomoa bastola yake akatazama pande zote kama kuna mtu karibu yao lakini hakukuwa na mtu yeyote mwenye silaha pale karibu

“A sniper” alisema Mathew

“Regina sikiliza kuna mdunguaji yuko sehemu anatushambulia.Ili tuokoke utafuata kile nitakachokuelekeza” alisema Mathew.Alifungua kiwambo cha bastola yake halafu akaachia risasi mbili hewani.Mlio ule wa risasi ulileta taharuki kubwa watu wakaanza kukimbia hovyo.Mathew akiwa amemshika mkono Regina

walitoka mbio wakiungana na watu wengine waliokuwa wanakimbia kunusuru maisha yao

“Umefanya kitu gani? Jombaa aliunguruma kama Simba.Sura yake ilifura hasira

“Haikuwa rahisi kuua watu wote watatu lakini nimeua mmoja.Katika harak........” Gosu Gosu alijitetea lakini ghafla akapigwa na kitu kizito akaanguka chini.

“Umeharibu misheni nzima.” alisema Jombaa

ENDELEA..............

Regina alianguka chini wakati wakikimbia kutokana na viatu virefu alivyokuwa amevaa.Mathew aligeuka haraka haraka akapata wazo.Aliisambaratisha kwa risasi taa kubwa ambayo ilitoa mwangaza eneo lile na kulifanya eneo la mbele liwe na mwangaza hafifu.Regina bado alikuwa chini akigugumia maumivu aliyoyapata baada ya kuanguka.Mathew alimvua viatu akavitupa, akamuinua

akamuweka beganai akaanza kukimbia naye kuelekea katika geti kuu la kuingilia katika ile baa.Kulikuwa na heka heka kila mtu akitaka kupita katika geti kuokoa maisha yake.

Baada ya kufanikiwa kuvuka geti,Mathew alichukua simu yake akampigia Ruby

“Ruby uko wapi? Aliuliza Mathew baada ya Ruby kupokea simu

“Tayari nimekwisha toka .Nielekeze ulipo tafadhali” alisema Ruby.

Mathew alimuelekeza Ruby uelekeo wake.Hakusimama aliendelea kukimbia kandoni mwa barabara.Mara ghafla ilifunga breki gari na mlango ukafunguliwa.

*“Get in quick!* ilisema sauti ya Ruby.

Mathew alimuingiza Regina garini naye akaingia Ruby akaliondoa gari kwa kasi huku wakiacha heka heka kubwa eneo lile.

Garini Regina alikuwa anatetemeka.Kile kilichotokea

kilimuogopesha mno.Mathew alikuwa makini sana kuhakikisha kuwa hawafuatiliwi.Alimpa maelekezo Ruby ya kutokwenda moja kwa moja katika makazi yao ili wajiridhishe kama hakuna anayewafuatilia.

“Mn..na..ni..p..p..peleka wapi? Aliuliza Regina huku akitetemeka.Hakuna aliyemjali.Mathew alikuwa makini kuchunguza kama wanafuatiliwa,huku Ruby akiwa makini na usukani.

Walizunguka mitaa kadhaa ya jiji la Arusha na baada ya kujiridhisha hawakuwa wanafuatiliwa walishika njia ya kuelekea katika makazi yao.

“Jamani mnanipeleka wapi? Aliuliza Regina huku akilia.Hakuna aliyemjibu.

Safari iliendelea kimya kimya hadi walipofika katika makazi yao.Regina alishushwa garini akaingizwa katika mojawapo ya chumba katika ile nyumba.

“Jamani naombeni msiniue tafadhali.Nitawapatia kiasi chochote cha fedha mnachokitaka” alilia Regina

“Shhhh !!! alisema Mathew akimfanyia ishara Regina akae kimya

“Pumzika,nitakuja kuzungumza nawe baada ya muda mfupi” alisema Mathew.Alisimama kwa sekunde kadhaa akamtazama Regina halafu akatoka mle chumbani akamfuata Ruby

“Pole sana Mathew” alisema Ruby ambaye alikuwa ameiinamia kompyuta yake

“Tangu tumetoka kule baa nimekuwa nikitafakari kuhusu tukio lile nimekos a jibu.Nani hasa alikuwa mlengwa? Ni mimi ? aliuliza Mathew

“Hapana Mathew.Mlengwa haukuwa wewe” alijibu Ruby na kumtaka avute kiti asogee karibu.

“Wakati tunaelekea Duma bar ile saa ambayo tulimpa Gosu Gosu iliwashwa na

kuiwezesha program yetu kuweza kunasa sauti zote za mazungumzo.Hiki ndicho alichokisema Gosu Gosu" alisema Ruby na kucheza sauti ya Gosu Gosu

*"Kazi imeanza"* Ilisema sauti ya Gosu Gosu

"Huu ulikuwa ni ujumbe kwetu kwamba kazi aliyotakiwa kuifanya usiku ule ilikuwa imeanza.Baada ya kuupata ujumbe ule niliendelea kuwafuatilia na safari yao iliishia Duma bar mahali ambako

tulikuwepo.Mara baada ya kufika pale Duma,alisikika Jombaa akimueleza Gosu Gosu kwamba kazi itafanyikia pale Duma bar” alisema Ruby na kucheza mazungumzo ya Gosu Gosu na Jombaa Mathew akayasikiliza.

“Baada ya hapo” Ruby aliendelea.

“Waliingia katika chumba ambamo kulikuwa na watu ambao sijui idadi yao.” Alisema Ruby akacheza mazungumzo yote ambayo program yake iliyanasa kupitia

ile saa ambayo alikuwa ameivaa Gosu Gosu.Mathew aliyasikiliza mazungumzo yale kwa umakini mkubwa.Alimtaka Ruby kurudia kucheza kipande Fulani cha mazungumzo ya Gosu Gosu

"*Haikuwa rahisi kuua watu wote watatu lakini nimeua mmoja.Katika harak........*"

"Hiyo ilikuwa ni sauti ya mwisho kurekodiwa na ile saa aliyoivaa Gosu Gosu.Baada ya kauli hiyo nimepoteza

mawasiliano na ile saa,hakuna kinachopatikana tena” alisema Ruby

“Sasa nimeelewa kila kitu kuhusiana na lile tukio.Walengwa walikuwa ni Regina na yule jamaa mwingine Amani.Hiyo ndiyo kazi ya pili ambayo Gosu Gosu alileta kuja kuifanya hapa Arusha.Hakujua kama mtu aliyetakiwa kumuua usiku ule ni Regina.Kama utakumbuka hawa jamaa hawakutaka kumueleza chochote hadi walipomfikisha eneo la tukio na kumuonesha mtu ambaye

anatakiwa amuue.Gosu Gosu aliponiona nikiwa katika ile meza pamoja na akina Regina alishtuka ndiyo maana katika mazungumzo haya yaliyorekodiwa alionesha kushtuka na anasikika akisema *Oh my God* kwa sauti ndogo.Nadhani ni baada ya kuniona mimi nikiwa na Regina.Hakutegemea kabisa" alisema Mathew

"Niliamini Gosu Gosu hatakubali kukuua hata kama kufanya hivyo kutamgharimu uhai wake hivyo niliwasha gari na kutoka nje nikitegemea

ndani ya muda mfupi kungetokea kizaa zaa mahali pale” alisema Ruby

“Hukufanya vibaya lakini ulipaswa kunitaarifu.Ni vipi kama muuaji angekuwa si Gosu Gosu? Tayari ningekwisha uawa muda huu.Katika mapambano kama haya hakuna taarifa ya kupuuza hata kidogo” alisema Mathew

“Mathew niliogopa kukujulisha ili wale jamaa wasishtuke kwa sababu wanaonekana walikuwa

wanamfuatilia Regina hadi wakajua kwamba yuko mahali pale akimsubiri mtu.Hata mlipokuwa mmekaa pale mezani walikuwa wanawafuatilia hivyo ningekushtua kuhusu kile kinachoendelea lazima ungeondoka na usingekubali kumuacha Regina lazima ungeondoka naye kumuokoa.Hiyo ingewapa picha wale jamaa kuwa wanafuatiliwa mipango yao hivyo kumuweka Gosu Gosu katika hatari kubwa" alisema Ruby

“Umesema mawasiliano na ile saa aliyoivaa Gosu Gosu yamekatika? Aliuliza Mathew

“Ndiyo yamekatika.Sauti ya mwisho kwa Gosu Gosu ni pale alipokiri kuwa haikuwa rahisi kuua watu wote lakini hakumaliza sentnsi yake mawasiliano yalikatika.Kuna mambo mawili ninayafikiria hapa.Moja,yawezekana wale jamaa walimgundua Gosu Gosu wakaichukua ile saa wakaiharibu au kuna uwezekano aliigongesha ile saa ukutani ikaharibika.” Alisema Ruby

“Sababu ya pili ninaweza kukubaliana nayo na kama ni hivyo basi watakuwa walimpiga na kitu akapoteza fahamu akaanguka ndipo saa ile ikaharibika.Ninaamini hivyo kwa sababu yule jamaa aliyekuwa anamuongoza Gosu Gosu alimtaka afanye shambulio pale atakapohesabu hadi tatu lakini Gosu Gosu hakusubiri yule jamaa amalize kuhesabu aliachia risasi na kumuua Amani.Risasi nyingine alipiga chupa za vinywaji mezani ili kunipa ishara kuwa niko katika

hatari.Alichokifanya Gosu Gosu hakijawafurahisha wale jamaa na kitamuweka katika hatari kubwa” alisema Mathew

“Nina wasi wasi sana na hatima ya Gosu Gosu.Wanaweza wakamuua” alisema Ruby

“Kumuua si rahisi kwani bado wanamuhitaji.Lazima ipo sababu ya kumtumia Gosu Gosu katika mauaji haya.Wapo watu wengi ambao wangeweza kuwatumia lakini walimchagua Gosu Gosu.Tuliweke pembeni kwanza hilo kwa muda

tutazame kile kinachoendelea" alisema Mathew

"Mathew hatuwezi kumuacha Gosu Gosu.Tulikuja huku Arusha kumuokoa na kumtoa katika hatari.Hatuwezi kumuacha katika mikono ya wale jamaa" alisema Ruby

"Hatuwezi kumtelekeza.Tutamuokoa lakini si sasa.Kwa wakati huu ninataka tujielekeze katika kujua kwa nini Regina anatakiwa kuuawa? Lazima tuipate sababu.Ni wakati wa kwenda kuzungumza naye"

“Unadhani ataweza kusema chochote kwa sasa baada ya kile kilichotokea kule bar? Lazima atakuwa katika mshtuko mkubwa.Nadhani tumpe muda ili kwa sasa tushughulikie suala la Gosu Gosu” alisema Ruby

“Hatuna muda wa kumpa.Atazungumza kila kitu na atazungumza sasa hivi.Kwa wakati huu kila sekunde ina maana kubwa sana kwetu” alisema Mathew huku akipiga hatua kuelekea chumbani alimo Regina ambaye alikuwa ameinama huku mikono yake

mwili ikiwa imeufunika uso.Alikuwa analia.Baada ya akina Mathew kuingia mle ndani aliinua uso akawatazama.Macho yake yalikuwa mekundu kutokana na kulia.

“Tafadhali naombeni mniambie chochote kile mnachokitaka kwangu nitawapatia.Semeni mnahitaji shillingi ngapi mniache niende ndugu zangu.Niko tayari kuwapa fedha zote zilizo katika akaunti yangu” alisema Regina.Mathew alimtazama akasema

“Tafadhali naomba uketi Regina” alisema Mathew

“Ee Mungu naomba uniondoe katika janga hili” alisema Regina huku akiketi.Baada ya dakika moja Mathew akasema

“Regina kwanza kabisa nakuomba ondoa hofu.Uko sehemu salama” alisema Mathew na kumfanya Regina amtazame kwa hasira

“Sehemu salama? Mmeniteka na kunileta hapa halafu mnasema niko sehemu salama? Alifoka

“Relax Regina.Take a deep breath” alisema Mathew

“Ninajilaumu sana kwa kuwaamini kumbe ni wauaji wakubwa nyie.Mmemuua Amani..” Regina alishindwa kujizuia akaangua kilio kikubwa.Mathew alimfuata akamshika bega Regina akausukuma mkono wake

“Don’t touch me ! alifoka

“Mathew tumpe muda atulize kichwa ndipo tuzungumze naye” alisema Ruby

“Hatuna muda.Atatueleza kila kitu sasa hivi” alisema Mathew huku akimtazama Regina kwa macho makali

“Regina naomba unisikilize” alisema Mathew lakini Regina aliendelea kulia.Mathew akamshika mikono akamnyanyua

“Regina usitake nikulazimishe unisikilize.Sipendi kumuumiza mwanamke lakini ukinilazimisha nitafanya hivyo.Utanisikiliza au nikulazimishe unisikilize?

Aliuliza Mathew.Regina hakujibu kitu alijitoa katika mikono ya Mathew halafu akaketi.Macho yalijaa machozi.Mathew naye aliketi.

“Regina pole sana kwa tukio lile.Naamini limekuumiza mno na kukushtua lakini hiki ni kipindi ambacho unapaswa kuwa jasiri sana” Mathew alinyamaza kwa sekunde chache.

“Kwanza kabisa naomba ondoa hofu.Hapa uko sehemu salama kabisa.”

“Ninyi ni akina nani? Aliuliza Regina

“Ninaitwa Mathew Mulumbi.Niliwahi kufanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania” alisema Mathew na kunyamaza baada ya Regina kuonesha mshtuko

“Umesema unaitwa nani? Aliuliza Regina

“Naitwa Mathew Mulumbi.”

“Sasa nimepata jibu.Nilipokuona tu nilianza kujiuliza nimewahi kukuona

wapi.Nini kinachoendelea? Aliuliza Regina

“Yule pale ni mwenzangu anaitwa Ruby” Mathew alimalizia utambulisho

“Nini kinaendelea hapa ndugu zangu? Aliuliza Regina

“Ahsante kwanza kwa kuamua kutusikiliza.Sasa tukazungumze” alisema Mathew wakatoka mle ndani wakaenda sebuleni.

“Regina narudia tena kukuomba ondoa hofu,uko

sehemu salama." Alisema Mathew

"Naomba mnieleze tafadhali nini kinaendelea? Kwa nini Amani ameuawa? Nani waliomuua? Aliuliza Regina.Mathew aliichukua bahasha akaifungua na kutoa picha akampatia Regina.

"Kabla hatujaanza mazungumzo yetu naomba uzitazame picha hizi halafu uniambie kama unawafahamu watu hawa pichani" alisema Mathew

Regina alizitazama picha zile moja baada ya nyingine kwa makini halafu akasema

“Hapa niliyeweza kumfahamu ni mheshimiwa Gavana Jackson Mzumile,hawa wengine siwafahamu.Halafu huyu mmoja mbona ka............”

“He’s dead.Picha yake nimeichukua katika chumba cha kuhifadhia maiti”

“Nini kinaendelea hapa jamani? Aliuliza Regina akionesha woga mkubwa.

“Una uhakika hawa wengine huwafahamu? Aliuliza Mathew

“Siwafahamu.Ni mtu mmoja tu ambaye namfahamu kama nilivyosema ambaye ni Gavana wa benki kuu.Ni mtu maarufu hakuna asiyemfahamu hapa nchini” alijibu Regina

“Tazama tena vizuri hizo picha” alisema Ruby

“Naombeni mniamini ndugu zangu.Kama ningewafahamu watu hawa

ningewaambia” alisema Regina

“Anganile Mwaikusa unamfahamu? Aliuliza Mathew

“Ni nani huyo? Aliuliza Regina

“Naomba jibu unamfahamu? Mathew aliuliza

“Hapana simfahamu”

“Una hakika? Aliuliza Mathew

“Ndiyo nina uhakika.Ni mara ya kwanza kulisikia jina

hilo.Ni nani huyo mtu? Aliuliza Regina

“Umewahi kuwasiliana na Gavana Jackson? Mathew aliuliza

“Gavana? Regina alionesha mshangao

“Ndiyo.Umewahi kuwasiliana naye? Mnafahamiana? aliuliza Mathew

“Hapana sifahamiani naye na wala hatujawahi kuwasiliana.Kuna nini kwani? Regina aliuliza

“Unaishi wapi hapa Arusha? Aliuliza Mathew

“Chama kimenipangishia nyumba Ngaramtoni karibu na ofisi yetu” alijibu Regina

“Unaishi na nani katika hiyo nyumba?

“Nina msaidizi mmoja na mlinzi mmoja.Wengine ni walinzi wa kampuni ya ulinzi ambao hulinda nymba yangu kwa zamu.”

“Mlinzi wako ulikuwa naye pale bar? Aliuliza Mathew

“Hapana sikuwa naye” alijibu Regina

“Yuko wapi?

“Aliniomba ruhusa jana aende kwao kwa dharura.Baba yake aligongwa na gari” alijibu Regina

“Msaidizi wako wa ndani anaitwa nani?

“Anaitwa Suzy”

“Good.” Alisema Mathew akamgekia Ruby

“Nahitaji zile video” alisema Mathew.Ruby aliiweka mezani kompyuta yake

akafungua faili ambalo lilikuwa na zile video za Regina akiwa mtupu.

“Tafadhali naomba utazame video hizi” alisema Mathew.Regina alisogea na kupatwa mshtuko mkubwa alipotazama video ya kwanza.

“Oh my God ! this is me ! Where did you get this? Aliuliza kwa ukali

“Relax Regina.Tazama video zote halafu tutazungumza” alisema Mathew.

Regina aliendelea kutazama video zile huku mwili ukimtetemeka.Alifuta machozi alipomaliza kuzitazama.

"Ninaapa sijawahi kupiga picha za namna hii.Mimi ni mtu ninayejiheshimu sana.Nina heshimika ndani na nje ya chama siwezi kufanya upuuzi kama huu.Naombeni mniambie tafadhali mmezitoa wapi video hizi zenye kudhalilisha utu wangu? Aliuliza Regina

“Huna haja ya kueleza Regina.Tunafahamu hujapiga picha hizi” alisema Mathew

“Ni nani aliyenichukua video hizi ? Alikuwa na malengo yapi? Ninyi mmezipata wapi? Aliuliza Regina maswali mfululizo akiwa na shauku ya kutaka kumfahamu mtu aliyemchukua video zile akiwa mtupu.Mathew hakumjibu.Alilifungua faili lingine lenye kichwa ALIOKUTANA NAO.

“Naomba uzitazame picha za watu hawa na uniambie kama unawafahamu” alisema Mathew.Regina alianza kuzipitia picha zile moja baada ya nyingine.

“Mungu wangu nini hiki kinaendelea? Hawa wote ninawafahamu” alisema Regina

“Nataka unithibitishie kama umekutana nao wote hivi karibuni” alisema Mathew

“Ndiyo nimekutana nao wote hivi karibuni.” Alisema Regina

“Good” alisema Mathew huku akilifunga lile faili akafungua folda lenye picha ambalo lilikuwa na picha za Regina zilizotoka katika kamera ya Anganile bandia,akamtaka Regina azitazame

“Hizi zote ni picha zangu.Mmezipata wapi? Aliuliza Regina

“Regina baada ya kukuonesha picha hizo sasa umefika wakati wa kufahamu kila kitu.Kwanza kabisa naomba ufahamu kuwa

umekuwa unafuatiliwa.Picha hizi zote na zile video tumezitoa kwa huyu jamaa ambaye tayari amefariki dunia.Aliuawa jana usiku.Inaonesha wazi huyu jamaa alikuwa anakufuatilia.Zile video zote zilichukuliwa kutoka katika kamera ya siri zilizofungwa katika nyumba unayoshi bila wewe kufahamu.Kupitia kamera hizo aliweza kufuatilia kila kitu ulichokuwa unakifanya mle chumbani lakini alivutiwa zaidi na hizi video ukiwa mtupu ndiyo

maana aliamua kuzihifadhi ingawa sielewi kwa nini alizihifadhi”

“Are you sure? Aliuliza Regina

“Ndiyo Regina” alijibu Mathew

“Inawezekanaje? Chumba changu huwa ninakifunga ninapotoka.Hata usafi hufanywa wakati nikiwepo.Wamewezaje kuingia ndani na kufunga hizo kamera? Suzy alikuwa wapi? Wale walinzi wanaolinda nyumba yangu walikuwa wapi

wasimuone huyo mtu aliyeingia na kufunga kamera? Aliuliza Regina

“Regina hicho ni kitu kidogo sana wala usishangae kimewezekanaje.Zama hizi watu wakitaka kukuchunguza kufuatilia mambo yako lazima watakupata tu.” Alisema Ruby

“Kwa nini anifuatilie? Aliuliza Regina

“Hilo swali tutalitafutia majibu sisi na wewe lakini uhakika mwingine ambao unatufanya tuamini kuwa huyu jamaa alikuwa

anakufuatilia ni hizi picha za hawa watu uliokutana nao.Kila uliyekutana naye alikuwa anampiga picha.Nahisi alikuwa anawachunguza ni akina nani.Jambo lingine ni hizi picha zako.Zinaonesha mchukuaji alizichukua akiwa ndani ya gari.Tulifanikiwa kuipata laini ya simu ya huyo jamaa ambayo ilisajiliwa kwa jina la Anganile Mwaikusa.Kitu cha kushangaza ni kwamba laini hiyo ya simu ilikuwa na namba moja tu ya Gavana wa benki kuu.Tuliweza pia kunasa

mazungumzo kati ya Gavana na huyu mtu ambaye baada ya kumchunguza tumegundua jina hilo la Anganile si lake.” Alisema Mathew akaichukua picha na kumuonesha Regina

“Huyu ndiye Anganile Mwaikusa ambaye kitambulisho chake kimetumika kusajili laini ya simu aliyokuwa anaitumia huyu jamaa ambaye mpaka sasa bado hatumfahamu jina lake ni nani .Tumemepa jina la Anganile bandia” alisema Mathew

“Simfahamu kabisa huyu Anganile” alisema Regina akiishika tena ile picha ya Anganile

Mathew alicheza mazungumzo ya Gavana na Anganile bandia.Regina aliyasikiliza kwa umakini mkubwa halafu akafuta machozi.

“Alitumwa mtu kuja Arusha kumuua Anganile bandia.Kwa bahati nzuri mtu aliyetumwa kuja kuifanya kazi hiyo ni kijana wangu na ndiye aliyejitahidi hadi akaipata laini

ya simu aliyokuwa anaitumia Anganile bandia pamoja na kadi yake ya kamera.Baada ya kufanya mauaji hayo alitakiwa kufanya tena mauaji mengine lakini hakuambiwa nani anatakiwa kuuawa.Sisi baada ya kuzipata picha zile zako tuliamua kuwa karibu yako kuchunguza kama kuna kitu unakifahamu kuhusiana na hawa watu watatu" alinyamaza kidogo halafu akaendelea.

"Ukiacha huyu Anganile bandia ,tumegundua kuna timu nyingine inayokufuatilia.Tunaamini

watu hao wanafuatilia mazungumzo yako yote ya simu na wanajua kila mahali uendako.Walifahamu kuwa unakwenda pale Duma bar na utakutana na Amani.Ilipangwa muuawe wewe na Amani.Kwa bahati nzuri mtu aliyetakiwa kufanya mauaji hayo ni huyo kijana wangu na ndiye aliyetusaidia tukaweza kuondoka pale salama.Kama si yeye tungeuawa wote” alisema Mathew

“Tulipokutana kwa nini hukunieleza kama tutauawa? Aliuliza Regina

“Nilifahamu kuna mauaji yanatakiwa kufanyika usiku wa leo ila sikujua kama watu wanaotakiwa kuuawa ni wewe na Amani” alijibu Mathew

“Huyo kijana wako yuko wapi sasa hivi? Aliuliza Regina

“Hatufahamu yuko wapi.Mawasiliano kati yetu naye yamepotea” alijibu Mathew.Kimya kifupi kilipita

“Regina hatari haijaisha.Mambo ndiyo kwanza yameanza.Watu wanaotaka kukuua wanafahamu uko hai

bado.Watakusaka kila kona,ardhini na angani hadi watakapohakikisha lengo lao limetimia.Sisi pia ambao tumekuokoa tumeingia katika hatari ingawa hatuna hofu kwa sababu ni maisha yetu tumeyazoea.Kwa sasa tunahitaji sana ushirikiano wako.Inawezekana hukujua kama unafuatiliwa,hukufahamu kama kuna mipango ya kukuua,na huwajui wanaotaka kukuua. Lazima ipo sababu kwa nini hawa watu wanakufuatilia na wanataka

kukuua? Tunaendelea kumfuatilia huyu Anganile bandia kujua kama kweli alitumwa na Gavana kuja kukufuatilia.Wakati tukiendelea na hilo zoezi nataka utusaidie kufahamu kwa nini wewe na Amani mlitakiwa kuuawa? Aliuliza Mathew.

Regina aliinamisha kichwa chini akazama mawazoni na alipoinua kichwa macho yake yalijaa machozi

“Sifahamu chochote kwa nini ninafutiliwa.Sijui kwa nini

wanataka kuniua" alisema Regina

"Regina tumeyatoa maisha yetu kukusaidia wewe. Tutakulinda kwa nguvu zetu zote lakini tunaomba na wewe utupe ushirikiano mkubwa ili tufahamu sababu ya wewe kutaka kuuawa.Unadhani kwa nini wanataka wewe na mwenzako Amani muuawe? Aliuliza Mathew

"Ndugu zangu sifahamu chochote.Sina ugomvi na mtu yeyote na sijui kwa nini

wanataka kuniua” alijibu Regina

“Regina lazima ipo sababu.Hawa wanaotaka kukuua si mtu mmoja.Wanaonekana ni mtandao mkubwa.Wametumia nguvu kubwa kuhakikisha wanatekeleza lengo lao hivyo lazima ipo sababu kubwa ya kufanya hivyo.Huwezi kutakiwa kuuawa bila sababu yoyote.Hebu jaribu kufikiri kwa kina ili tufahamu nini ambacho kinaweza kusababisha ukauawa? Aliuliza Mathew

“Ndugu zangu sifahamu chochote.Mkiwapata hao wanaotaka kuniua watawaeleza kwa nini wanataka kuniua.Sababu wanayo wenyewe” alisema Regina.

“Regina wewe ndiye utakayetusaidia kuwafahamu hao watu ni akina nani kwa kutuambia nini sababu ya wewe kutakiwa kuuawa” Mathew aliendelea kusisitiza

“Jamani naombeni mniamini.Mimi sifahamu chochote.Watafuteni hao watu

watawaeleza kwa nini wanataka kuniua” alisema Regina.Kimya kikatawala

“Naombeni mnisaidie simu.I need to call someone” alisema Regina

“Regina kwa sasa hautaweza kuwasiliana na mtu yeyote yule.Watu wale wanaokutafuta wanakufuatilia na watafahamu kuwa uko hapa” alisema Mathew

“Nataka nimuondoe hofu mume wangu kuwa niko salama.Naamini hadi muda

huu atakuwa amezipata taarifa" alisema Regina

"Tutatafuta namna ya kuwasiliana na mume wako kumjulisha kuwa uko salama lakini si kwa kumpigia simu.Kwa mume wako ni sehemu ya kwanza ambayo wataanza kukutafutia kwa sababu wanaamini lazima utampigia kumjulisha uko salama.Kwa sasa ninakupa nafasi ya kutafakari kwa kina kwa nini hawa watu wanataka kukuua.Nitazungumza nawe tena baadae naamini utakuwa tayari na jibu.Ruby mrudishe

Regina chumbani.” Alisema Mathew.

Ruby alimpeleka Regina chumbani halafu akareja sebuleni.

“Kuna kitu anakifahamu huyu mwanamke lakini hataki kukisema” alisema Mathew

“Hata mimi nimegundua kitu hicho” aliongeza Ruby

“Tumpe muda atulize akili yake halafu tutamuhoji tena.Ipo sababu kubwa ya kutaka kumuua.Tukiachana na hilo kwa muda nataka tugeukie

suala la Gosu Gosu.Bado yuko katika hatari.Lazima jitihada zifanywe haraka kuhakikisha tunampata na kumuondoa katika hatari inayomkabili.Nataka ufuatilie ile simu ya Gosu Gosu tufahamu mahali alipokuwa kutwa nzima ya leo .Ninataka kwenda huko" alisema Mathew

"Mathew unadhani Gosu Gosu atakuwa huko? Aliuliza Ruby huku akianza kucheza na kompyuta yake

"Sina hakika lakini ni mahali alikofikia alipoletwa

hapa Arusha.NI sehemu ya kwanza kabisa ya kumtafutia Gosu Gosu.” Alijibu Mathew

“Sawa ninakutumia ramani katika simu yako ambayo itakufikisha mahali alipokuwa Gosu Gosu kwa siku nzima ya leo” alisema Ruby na baada ya muda mfupi ukaingia ujumbe katika simu ya Mathew akaufungua.Ilikuwa ni ramani ya jiji la Arusha ikionesha mahali alipokuwa Gosu Gosu kwa siku nzima.

“Chukua bastola hii,hakikisha Regina anakuwa

salama.Usipokee simu yoyote zaidi ya nitakayokupigia mimi” alisema Mathew na kumpatia Ruby bastola yake

“Unakwenda sehemu ya hatari Mathew lazima uwe na silaha.”alisema Ruby

“Usihofu Ruby.Nitakuwa salama.Endelea kuchimba zaidi kama utapata taarifa za hawa watu tunaowatafuta” alisema Mathew akatoka akaingia garini akaondoka

“Hili jambo si dogo.Ni jambo kubwa.Lazima ipo sababu kubwa ya kutaka

kumuua Regina.Lazima ataeleza kila kitu na kama akiendelea kuwa mbishi nitatumia hata nguvu.Kwa sasa ngoja nikapambane kumtafuta Gosu Gosu” aliwaza Mathew akiwa garini

**************

Ramani aliyopewa na Ruby, ilimuongoza Mathew kufika hadi katika nyumba ambayo aliamini ndimo alimokuwa akiishi Gosu

Gosu.Aliipita taratibu nyumba ile huku akiichuguza akaenda kuegesha gari mita kadhaa kutoka katika ile nyumba.Alishuka garini kisha kwa tahadhari alipiga hatua kurejea katika ile nyumba.Mtaa ulikuwa umetulia sana.Alilifikia geti akakutana na kufuli kubwa ishara kuwa wahusika hawakuwepo.Alitazama pande zote kama kuna mtu yeyote karibu lakini hakukuwa na mtu.Alirudi nyuma halafu akaruka kama Kima akalikamata geti kwa

juu,akajiinua akaweza kutazama ndani.Hakukuwa na dalili yoyote ya kuwepo mtu mle ndani.Ni taa moja tu iliyokuwa mbele ya ile nyumba ilikuwa inawaka.Mathew alijirusha ndani na kutua kitaalamu bila kutoa kishindo kikubwa.Hakupoteza muda akatembea kwa tahadhari kubwa hadi katika kibaraza.Alikinyonga kitasa mlango ulikuwa umefungwa.Alitoa kifaa chake maalum cha kufunguliwa vitasa akachokonoa kitaa kile taratibu kikafunguka

akaufungua mlango akaingia ndani.

Nyumba ilikuwa kimya sana.Akiwa na tochi ndogo alikagua pale sebuleni.Kulikuwa na sofa kuu kuu na kabati ambalo halikuwa na kitu chochote.Vichungi vya sigara vilitapakaa kila sehemu.

“Hii nyumba kweli wanaishi wazee wa kazi” aliwaza Mathew akatoka pale sebuleni akaingia katika moja ya chumba.Kilikuwa kikubwa chenye vitanda vinne.Aliingia

akachunguza lakini kilijaa harufu ya bangi.

“Hakuna kitu humu” aliwaza akatoka akingia katika chumba kingine kizuri ambacho kilijitosheleza kila kitu.Kilikuwa kisafi kupita vile alivyoingia

‘Nadhani humu ndimo alimokuwa analala Gosu Gosu” aliwaza akaendelea kuchunguza.Hakupata chochote akatoka akaenda katika chumba kingine.Alijaribu kufungua mlango ulikuwa umefungwa

kwa funguo.Kwa kutumia kile kifaa chake alifungua ule mlango akaingia ndani.Chumba kilikuwa na vitu vingi.Kulikuwa na kabati kubwa la chuma lililofungwa kwa kufuli kubwa.Alilifungua kufuli lile na ndani ya kabati alikuta kuna silaha mbali mbali.Kulikuwa na bunduki,bastola,fulana za kuzuia risasi,sare za jeshi la polisi pamoja na mabomu sita ya kurusha kwa mkono.Upande wa chini wa lile kabati kulikuwa na zana

mbali mbali kwa ajili ya kuvunjia makufuli na milango.

“Hawa jamaa wamejiandaa vya kutosha” aliwaza akalifunga lile kabati na kwenda katika kabati lingine ambamo kulikuwa na nguo.Wakati akiendelea kupekua alisikia muungurumo wa gari.Alifunua pazia akachungulia nje aliwaona watu wawili wakishuka katika lile gari.Alilifungua lile kabati kubwa la chuma akachukua bastola akaichunguza ilikuwa na risasi za kutosha,akalifunga lile kabati kama lilivyokuwa

akatoka ndani ya kile chumba akaenda kujificha katika chumba kilichokuwa kinatumika kama jiko.

Mlango wa sebuleni ulifunguliwa wale jamaa wakaingia ndani wakawasha taa.

“Ni mara ya kwanza leo kumsikia Jombaa akikiri kazi imeharibika.” alisema mmoja wa wale jamaa akiwa ameketi sofani

“Tuachane na hayo.Nenda kaanze kupakia zana tuondoke mahali hapa tumuwahi

Jombaa.Mimi nakwenda kuoga nahisi joto.” alisema mmoja wa wale jamaa

“Sawa Jeraa” alijibu mwenzake akainuka akaingia katika chumba kile kilichokuwa na silaha.Mathew akiwa mle jikoni alisikia maji yakimwagika bafuni.Alitoka mle jikoni kwa tahadhari kubwa akatembea kuelekea katika kile chumba zilimo silaha.Aliufungua mlango taratibu.Jamaa aliyekuwa ndani alidhani mwenzake ndiye aliyeingia hivyo hakujisumbua kutazama

mlangoni.Aliendelea na zoezi la kupakia silaha katika sanduku kubwa la chuma.Mathew baada ya kuufunga mlango alikohoa kidogo.Jamaa aliinua kichwa akakutana na mdomo wa bastola.

“Shhhh !!! alisema Mathew halafu akamsogelea karibu akamsemesha kwa sauti ndogo.

“Endelea na kazi yako kimya kimya.Ukijaribu kufungua mdomo wako nitakufumua kwa risasi”

alisema Mathew.Huku akitetemeka yule jamaa aliendelea kupanga silaha katika lile sanduku huku Mathew akimtazama kwa makini kuhakikisha hana madhara yoyote.Uso wake ulilowa jasho.

Wakati akiendelea kupakia, vilisikika vishindo vya mtu akielekea katika kile chumba.Mathew alisogea pembeni ya mlango ili kumpisha yule jamaa aliyekuwa anakuja.Kitasa cha mlango kilinyongwa na kabla jamaa hajaingia yule

mwenzake aliyekuwa ndani alipiga ukelele

“Jera kimbia !

Yule jamaa aliyekuwa nje hakuelewa nini mwenzake alikimaanisha.Alichomoa bastola yake akaingia ndani kwa kasi.

“Kuna nini Muddy? Aliuliza

“Weka silaha yako chini tafadhali ! Sauti ilimuamuru kutoka pembeni ya mlango.Jera alikuwa

anatazama na mdomo wa bastola.

“Wewe ni n…” hakumaliza sentensi yake Mathew akaachia risasi iliyompata Jera katika paja la mguu wa kulia.Alichukua maamuzi yale baada ya kukiona kitendo ambacho Jera alitaka kukifanya.Kidole chake tayari kilikwisha gusa kiwambo cha bastola aliyokuwa ameishika mkononi.Aligaa gaa chini huku damu ikimvuja.Mathew alisogea karibu akaipiga teke bastola ile ikaenda chini ya uvungu wa kitanda.

“Muddy haraka sana muinue mwenzako twende nje” alisema Mathew

“Siendi kokote.Niue humu humu ndani ! alifoka Jera huku akigugumia kwa maumivu.

“Huyu haoneshi kama anatania.Ana maanisha kile akisemacho.Tayari ni mzigo na sina sehemu ya kumpeleka.Huyu maisha yake yanaishia hapa nitaondoka na mwenzake ambaye atanisaidia kujua mahali aliko Gosu Gosu” aliwaza Mathew.Bila huruma

aliizinga bastola yake.Risasi tatu mfululizo zilizama katika kifua cha Jera.

“Inuka haraka sana ! Mathew alimuamuru Muddy.Hakufanya ubishi kwani alimshuhudia mwenzake akikata roho.Aliogopa sana.Mathew alimuamuru aongoze kutoka nje akamtaka aifunge nyumba.Geti halikuwa limefungwa walitoka nje akamuamuru kulifunga kwa kufuli.Tayari kulikuwa na watu wachache waliokuwa wametoka nje ya nyumba zao

baada ya kusikia ile milio ya risasi.Mathew hakuwajali alimuongoza Muddy hadi katika gari lake akamfungulia mlango akaingia naye akapanda akaliondoa gari kwa kasi.

"Brother naomba unisamehe usiniue tafadhali" aliomba Muddy wakiwa garini.Mathew ambaye aliendesha gari kwa kutuia mkono mmoja huku mkono mwingine akiwa ameishika bastola hakumjibu kitu alijielekeza mbele huku akiwa makini kuhakikisha hakuna

anayewafuatilia.Karibu na baa moja aliegesha gari.Alihakikisha hakuna gari linalowafuata kwa nyuma.

“Jina lako  nani? Aliuliza Mathew

“Naitwa Muddy”

“Muddy umeona nilichomfanya mwenzako.Nilimtoa uhai mbele yako.Nilimuua kwa sababu ya kiburi chake.Wewe sintakuua lakini nitafanya hivyo kama utajaribu kwenda kinyume na vile nitakavyo

mimi.Umenilelewa? aliuliza Mathew kwa ukali.

“Nimekuelewa brother.Naomba usiniue tafadhali”

“Sintakuua.Nataka uniambie nini hasa shughuli zenu? Aliuliza Mathew

“Sisi tunafanya kazi za kukodishwa brother”

“Kazi zipi? Alifoka Mathew

“Kazi za kutumia silaha.Kuvamia na kupora au kuua”

“Ninyi ni majambazi” alisema Mathew na Muddy akawa kimya.

“Silaha zile mlikuwa mnazipeleka wapi? Aliuliza Mathew

“Tulikuwa tunaziondoa pale ndani”

“Mlikuwa mnazipeleka wapi? Kuna kazi mnakwenda kuifanya?

“Hapana.Tulielekezwa na mkuu wetu tuziondoe”

“Mkuu wenu anaitwa nani? Aliuliza Mathew

“Anaitwa Jombaa”

“Kwa nini akataka mziondoe zile silaha pale katika ile nyumba?

“Anahofu tungeweza kuvamiwa muda wowote”

“Kuvamiwa na nani? Aliuliza Mathew lakini Muddy hakujibu

“Muddy nakuuliza mna hofu ya kuvamiwa na nani?

“Hakutuambia tutavamiwa na nani.Sisi tunafuata maelekezo yake” alijibu Muddy

“Aliwapa maelekezo ya kupeleka wapi zile silaha baada ya kuzitoa katika ile nyumba? Aliuliza Mathew

“Alitueleza tuzipeleke maskani B” alijibu Muddy

“Nataka kufahamu mahali aliko huyo kiongozi wenu Jombaa” alisema Mathew

“Alisema tutamkuta maskani B”

“Nipeleke huko haraka sana” alisema Mathew

“Brother hapo ni mahali pa hatari sana.Sikushauri uende huko” alisema Muddy.

Mathew alimtazama Muddy kwa sekunde kadhaa halafu akawasha gari.

“Nipeleke maskani B nikaonane na Jombaa” alisema Mathew sura yake ikionesha hakuwa na masihara hata kidogo.

Muddy alimuelekeza Mathew njia ya kupita kuelekea Maskani B aliko Jombaa

**************

Muddy alimtaka Mathew asimamishe gari mara walipoingia katika mtaa ilipo maskani B.

"Maskani B ni nyumba ya nne kutoka hapa" alisema Muddy

"Kwa nini unataka tusimame hapa? Ninataka ukanioneshe ilipo hiyo nyumba"alisema Mathew

"Brother sikushauri twende huko.Ni mahali pa

hatari sana.Wote wawili tunaweza kupoteza maisha.” Alisema Muddy

“Kwa nini ni sehemu hatari? Mathew aliuliza

“Ni hatari kwa kuwa majambazi wote wa jiji la Arusha hukusanyika hapo.Mipango yote mikubwa ya ujambazi hufanyikia hapo.Ni mahali pa siri sana ambako hata polisi hawapajui.Haruhusiwi kungia mtu asiyefahamika.Wakikuona watakuua na wataniua mimi

pia ambaye nimekupeleka” alisema Muddy

“Unadhani kuna njia nyingine yoyote ya kumpata Jombaa zaidi ya kumfuata katika hiyo nyumba? Kama unadhani ipo namna nyingine ya kuweza kumpata niambie tafadhali ama sivyo utaniongoza kwenda ndani ya hiyo nyumba”Alisema Mathew

“Nitampigia simu na kumtaka atoke nje tuzungumze”

“Utamshawishije hadi akuelewe na atoke nje? Aliuliza Mathew

“Nitamwambia kuna jambo nataka kuzungumza naye faragha.Nitasema kuna kitu tumekigundua cha muhimu sana.Tutalisogeza gari hadi katika mti wa Zambarau ambao uko karibu na ile nyumba.Wewe utajibanza nyuma ya mti atakapotokea tu utamchukua” alisema Muddy.Mathew alifikiri kidogo halafu akasema

“Sawa mpango mzuri.Fahamu kuwa ninayemtaka ni Jombaa pekee.Nikimpata huyo wewe nitakuacha huru lakini ukijaribu kutaka kuharibu mpango huu nitakumaliza wewe kwanza kama nilivyommaliza mwenzako” alisema Mathew

“Siwezi kuharibu brother naomba uniamini.” Alisema Muddy.Mathew aliwasha gari na kuendesha hadi katika mti wa Zambarau alioelekezwa na Muddy.Alikuwa makini sana.Muddy alichukua simu

yake akaitafuta namba ya Jombaa akampigia

“Muddy.Kazi imemalizika? Aliuliza Jombaa

“Kazi imekamilika lakini kuna jambo muhimu nataka kuzungumza nawe faragha”alisema Muddy

“Mko wapi kwa sasa? Aliuliza Jombaa

“Tuko hapa Mzambarauni.Tunakuomba mara moja” alisema Muddy

“Sawa ninakuja” alisema Jombaa

Baada ya dakika tano mtu mmoja alionekana akipiga hatua ndefu kuelekea Mzambarauni huku akigeuka na kutazama nyuma mara kwa mara.

“Jombaa yule pale anakuja” alisema Muddy.

“Una hakika ni yeye? Aliuliza Mathew

“Ndiyo.Ninafahamu mwendo wake” alijibu Muddy.Mathew alishuka garini akaenda kujificha nyuma ya mzambarau.Mahali walipokuwa hapakuwa na

mwanga wa kutosha hivyo ilikuwa rahisi kwao kumuona Jombaa akielekea katika lile gari.Alipolikaribia Muddy naye alishuka garini

“Jombaa” aliita Muddy

“Kuna nini Muddy? Hili gari mmelitoa wapi? Aliuliza Jombaa

“Samahani Jombaa kwa kukusumbua”

“Kuna nini kimetokea? Unanipa wasi wasi sana.Jera yuko wapi? Aliuliza Jombaa.Muddy aligeuza

shingo kutazama katika ule mti wa Zambarau.

“Kuna nini Muddy? Aliiuliza Jombaa huku akiitoa bastola yake akayaelekeza macho yake kule Mzambarauni

“Yule bazazi amekwisha mpa Jombaa ishara Fulani.Natakiwa kufanya jambo hapa haraka sana” aliwaza Mathew na kugeuka kwa kasi ya ajabu akaachia risasi iliyompata Jombaa katika paja la mguu wa kulia akaanguka chini.Muddy alipoona Jombaa ameanguka

chini baada ya kupigwa risasi alitimua mbio.Mathew hakumjali kwani hakuwa na shida naye tena.Aliyemuhitaji ni Jombaa.Alitoka mbio nyuma ya mzambarau akamfuata Jombaa kwa tahadhari kubwa.Jombaa aliyekuwa ameanguka chini alimuona Mathew akimuendea akajiinua ili achukue bastola yake iliyoanguka mbali kidogo na mahali alipoanguka.Mathew alikiona kitendo kile akaruka kama Nyani na kumrukia Jombaa teke zito lililomrusha mbali

zaidi na ile bastola.Mathew hakumpa Jombaa nafasi alimuinua akamtandika kichwa kizito.Jombaa mtu mwenye mwili mwembamba alianguka kama furushi.Hakuwa na fahamu.Mathew alimuinua akafungua mlango akamuingiza garini naye akarukia katika usukani akaligeuza gari akaliondoa kwa kasi kubwa.

Mlio ule wa risasi kutoka katika ile bastola aliyokuwa nayo Mathew uliwashtua watu waliokuwa katika ile nyumba

alimotoka Jombaa.Mlio ule uliwapa hofu kubwa hivyo hawakutoka kwa haraka.Ni Muddy aliyeingia ndani kwa kasi kubwa ndiye aliyewashtua kuwa Jombaa amepigwa risasi.Walimuuliza amepigwa risasi na nani lakini naye hakumfahamu mtu huyo.Hii iliwafanya watu wale waliokuwamo ndani ya ile Maskani B watoke kwa tahadhari kubwa sana.Walichelewa kwani wakati wanatoka tayari Mathew Mulumbi alikwisha toweka.Muddy aliwaongoza

hadi katika mzambarau mahali alikopigwa risasi Jombaa.Walifanikiwa kuipata bastola ya Jombaa lakini mwenyewe hawakumpata.Walichanganyikiwa.Walijaribu kuipiga simu yake iliita mara moja halafu ikakatwa na kuzimwa kabisa.

Haraka haraka waliingia katika magari mawili na kujaribu kumfuatilia mtu aliyemtorosha Jombaa japo hawakuwa na uhakika mahali alikoelekea huyo mtu.

***************

Mathew alirejea katika makazi yao ya muda.Ruby alimfungulia geti akaingiza gari ndani.Alishuka garini akiwa kifua wazi huku mikono yake ikiwa imeloa damu.Ruby alishtuka mno

“Mathew are you okay? Aliuliza Ruby kwa wasiwasi

“Usihofu Ruby niko salama” alijibu Mathew

“Damu hiyo yote iliyokutapakaa mwilini imetoka wapi? Are you hurt?

Aliuliza Ruby.Mathew hakumjibu bali alifungua mlango wa gari akawasha taa ya ndani na Ruby akamshuhudia mtu akiwa amelala katika kiti cha nyuma hana fahamu.

“Huyu ndiye Jombaa ambaye alisimamia ule mpango wote wa mauaji” alisema Mathew akamshusha Jombaa akamuingiza ndani.Alimuingiza katika chumba kimoja kilichokuwa tupu akamlaza sakafuni.

“Ni mzima huyu? Aliuliza Ruby.

“Ni mzima lakini tunahitaji kumpata daktari wa kumuhudumia.Amepoteza damu nyingi” alisema Mathew

“Huku Arusha tutampata wapi daktari? Aliuliza Ruby.Mathew hakumjibu alichukua simu yake akaitafuta namba ya Dkt Phillip ambaye ni rafiki yake na ambaye ndiye huwa anamtumia pale anapohitaji msaada wa kitabibu hasa akiwa katika misheni zake.

“Mulumbi habari za usiku huu? Aliuliza Dkt Philip baada ya kupokea simu

“Dkt Philip ninahitaji msaada wako wa haraka” alisema Mathew

“Nini tena Mathew? Aliuliza Dkt Philip

“Niko Arusha,ninahitaji msaada wa daktari.Kuna mtu amepigwa risasi mguuni hana fahamu.Amepoteza damu nyingi.Mtu huyo anazo taarifa muhimu sana ambazo ninazihitaji.Sina daktari yeyote ninayemfahamu kwa hapa

Arusha ndiyo maana nimekuja kwako unisaidie.Unamfahamu daktari yeyote ninayeweza kumpata kwa usiku huu akanisaidia? Aliuliza Mathew.Dr Philip alifikiri kidogo halafu akasema

“Ninaye rafiki yangu mmoja anaitwa Dkt Linus Albert.Ni daktari bingwa mstaafu wa upasuaji.Kwa sasa baada ya kustaafu amekuwa akiitwa kufanya upasuaji katika hospitali mbali mbali ndani na hata nje ya nchi.Naamini hataweza

kukataa lakini malipo yake ni makubwa" alisema Dkt Philip

"Dkt Philip usijali kuhusu fedha.Kiasi chochote anachokihitaji nitampatia" alisema Mathew

"Sawa Mathew ngoja nimpigia nimuombe aje akusaidie" alisema Dkt Philip na kukata simu

"Kuna chochote umekipata? Aliuliza Mathew

"Hapana bado sijapata kitu kingine"

"Regina anaendeleaje?

“Bado yuko chumbani.Bado amechanganyikiwa.” Alijibu Ruby.

Mathew alienda katika chumba alimo Regina ambaye alishtuka mno alipomuona Mathew akiwa kifua wazi na mwili wake ukiwa umetapakaa damu.

“Regina nakuomba tafadhali” alisema Mathew

“Kuna nini? Aliuliza Regina akionesha woga

“Kuna kitu nahitaji ukione” alisema Mathew.Regina aliinuka akamfuta Mathew wakaingia katika chumba alimokuwa amewekwa Jombaa.Regina alishtuka sana

“Is he alive? Aliuliza

“Unaweza ukamtambua mtu huyu? Aliuliza Mathew huku akimgeuza Jombaa ili Regina amuone vizuri usoni

“Hapana simfahamu huyu mtu.Ni mara ya kwanza ninamuona” alisema Regina

“Huyu anaitwa JOmbaa.Ni jambazi sugu hapa Arusha na ukanda wote wa Kaskazini mwa nchi.Huyu ndiye aliyeratibu mpango wote wa kukuua wewe na Amani” alisema Mathew.Regina alishindwa kujizuia akaanza kulia.Mathew alimtoa mle chumbani na kumrejesha chumbani kwake.Mara simu yake iliita alikuwa ni Dkt Phillip

“Dkt Philip kuna mafanikio? Aliuliza Mathew

“Ndiyo Mathew nimefanikkiwa kuzungumza naye.Amekubali”

“Good.Anahitaji kiasi gani cha fedha? Aliuliza Mathew.

“Ninakutumia namba yake ya simu ili umpigie mtaelewana lakini kiasi alichokitaja ni kikubwa”

“Ahsante sana Dkt Philip.Pesa si kitu nitampa kiasi anachohitaji” alisema Mathew akakata simu.Baada ya muda mfupi ukaingia ujumbe katika simu yake kutoka kwa Dkt Philip.Ilikuwa

ni namba ya simu ya Dkt Linus.Bila kupoteza muda Mathew akampigia.

“Hallow” ilisema sauti nzito upande wa pili

“Natumai nazungumza na Dkt Linus Albert” alisema Mathew

“Ndiyo.Wewe nani mwenzangu? Aliuliza Dkt Linus

“Nimepewa namba yako na Dkt Philip ambaye umezungumza naye muda si mrefu”

“Ndiyo nimezungumza na Dkt Philip.Wewe uko wapi? Aliuliza Dkt Linus

“Nielekeze ulipo tafadhali nikufuate” alisema Mathew

“Usihofu ndugu yangu.Niambie mahali ulipo nikufuate mara moja.Dkt Philip amenielewesha kila kitu”

“Dkt Linus mimi si mwenyeji sana wa maeneo haya sina hakika kama ninaweza kukuelekeza vizuri.” Alisema Mathew.Dkt Linus

alimuelekeza mahali ambako alitaka wakutane.

“Ninamfuata Dkt Linus.Kuwa makini sana na huyu jamaa kama atazinduka.He’ a killer” Mathew alimpa Ruby tahadhari kisha akapanda garini akamfuata Dkt Linus.

***************

Ruby alifungua geti na gari mbili zikaingia ndani.Moja ilikuwa ya Mathew nyingine ya Dkt Linus.Alishuka garini akiwa na sanduku lililosheheni dawa na vifaa mbali mbali kwani Dkt Philip alikwisha mueleza tatizo la mgonjwa anayetakiwa kumuhudumia.Hakukuwa na sekunde ya kupoteza,Mathew alimpeleka Dkt Linus katika chumba alimo Jombaa.Dkt Linus aliomba meza ambayo angeitumia katika upasuaji ambayo ililetwa kwa haraka

Jombaa akalazwa juu yake.Dkt Linus alianza kazi.

Haikumchukua Dkt Linus muda mrefu kuitoa ile risasi katika paja la Jombaa.Baada ya kumaliza upasuaji aliondoka kufuata damu kwani Jombaa alihitaji kuongezewa damu.Wakati wakimsubiri Dkt Linus arejee,Mathew alimtuma Ruby akamuite Regina.

“Tayari amefanyiwa upasuaji tunasubiri akizunduka tutamuhoji ili kuwafahamu watu waliomtuma afanye mauaji

yale.Wakati tunasubiri azinduke ninataka kuzungumza nawe tena.” Alisema Mathew

“Nimetoka sehemu ya hatari sana usiku huu ambako ndiko nimemtoa huyu Jombaa.Ni kambi ya majambazi sugu.Nimeyafanya haya yote kwa ajili ya mambo mawili.Kwanza kufahamu aliko mwenzetu na pili kufahamu watu ambao wanataka kukuua. Pamoja na kumpata huyu mratibu mkuu wa mpango huo wa mauaji lakini bado hatutaweza kujua

kwa nini wanataka kukuua. Bado tunahitaji sana msaada wako.Tumekupa muda wa kutafakari kujua kwa nini hawa watu wanataka kukuua.Nini umekipata katika tafakri yako?” aliuliza Mathew

“Jamani ninawashkuru sana kwa kuniokoa katika shambulio lile lakini nimetafakari mno nini hasa sababu ya wao kutaka kuniua nimekosa jibu” alisema Regina

“Regina nimekueleza kuwa huyu mtu ambaye nimetoka kumchukua usiku huu ni

jambazi sugu.Ana mtandao mkubwa na ambao hivi sasa wananisaka.Wakifahamu niko hapa watavamia na hakuna atakayetoka hai.Tunahatarisha maisha yetu hivi si kwa ajili yetu bali kwa ajili yako.Nina uhakika mkubwa wa kumpata mwenzetu lakini vipi kuhusu wewe?Utaendelea kuwa salama? Sina hakika kama utamaliza siku mbili ukiwa bado hai.Jamaa watakumaliza.Ninafahamu unajua sababu kwa nini wanataka kukuua lakini unaogopa kusema.Uoga wako

ndiyo kifo chako.” Alisema Mathew.Zilipita dakika mbili Regina akasema

“Hapana sifahamu sababu kwa nini wanataka kuniua”

Mathew alimtazama kwa makini halafu akasema

“Nimekuelewa hutaki kutoa ushirikiano kwetu.Kama ni hivyo hatuna haja ya kukuweka hapa.Nitakurudisha nyumbani kwako.Jiandae tafadhali nikurejeshe nyumbani kwako sisi tutaendelea kumtafuta mwenzetu na tukimpata basi

hatutachimba zaidi suala hili” alisema Mathew akainuka akaenda katika chumba alimo Jombaa ambaye bado hakuwa amezinduka.Alirejea tena sebuleni

“Twende tuondoke” alisema Mathew.Regina alimuaga Ruby akaingia garini,Mathew akaliondoa gari.

***************

Kwa maelekezo ya Regina walifika katika nyumba anayoishi eneola Ngaramtoni.

“Regina umefanya kosa kubwa sana kukataa kushirikiana nasi.Nakutakia kile la heri” alisema Mathew.Regina hakujibu kitu aliufungua mlango akashuka.Kabla hajalifikia geti ilitokea piki piki moja kubwa yenye rangi nyeusi.Kasi iliyokuja nayo ilimfanya Regina asimame akageuka kuitazama na ndipo Mathew aliposhuhudia kitu.Jamaa aliyekuwa amekaa nyuma

aliinuka kidogo huku mkononi akiwa na bunduki ndogo.Kwa kasi ya aina yake alifungua mlango wa gari akamkimbilia Regina,akamrukia akamuangusha chini halafu akageuka haraka akaachia risasi akamlenga yule dereva aliyekuwa amevaa kofia ngumu.Risasi mbili alizopiga Mathew zilivunja kioo cha mbele cha ile kofia ngumu na kupenya moja kwa moja katika kichwa cha yule jamaa.Piki piki iliyumba na kuanguka kwa kishindo katika mtaro.Jamaa aliyekuwa amekaa nyuma

ambaye alikuwa na bunduki ndogo aliruka kiufundi sana lakini Mathew alikuwa mwepesi zaidi yake akamtandika risasi kadhaa kutoka katika bastola yake jamaa akaenda chini.Alinyanyuka pale chini akawafuata wale jamaa kwa tahadhari kubwa.Alijiridhisha wale jamaa wote hawakuwa na uhai.Alirejea mahali alipokuwa ameanguka Regina ambaye alikuwa anatetemeka.

“Regina ingia ndani tafadhali” alisema

Mathew.Regina alikuwa anatetemeka.

“Wale watu ni akina nani? Aliuliza

“Sifahamu lakini walikuwa na silaha.Inaonesha walikuwa na lengo baya.Regina ingia ndani tafadhali.Hapa nje si mahali salama kwako” alisema Mathew huku akienda katika geti ambalo halikuwa limefungwa.Alilisukuma na ndipo alipokutana na kitu cha kutisha.Watu wawili waliovalia sare za kampuni binafsi ya ulinzi walikuwa wamelala

chini.Hawakuwa na uhai.Mathew alimuinua Regina akampeleka getini akamuonesha kile kilichotokea mle ndani.Regina alishindwa kuvumilia akaangua kilio.

"Regina kulia hakutakusaidia kitu chochote.Ni juu yako sasa kuchagua aidha kama unataka kubaki hapa au vinginevyo" alisema Mathew

"Tafadhali usiniache hapa" alilia Regina

"Kama unataka kuongozana nami ukubali

kushirikiana nasi.Kama bado unaendelea na msimamo wako wa kutokusema chochote sintakuwa na namna ya kukusaidia,nitakuacha hapa”

“Tafadhali kaka nakuomba unisaidie.Usiniache hapa.” Alilia Regina.Mathew alimshika mkono wakaingia ndani ya gari na kuondoka kwa kasi kubwa.Regina aliinama akilia.

***************

Mathew na Regina walirejea katika makazi yao.Regina bado aliendelea kulia.Picha ya kile alichokishuhudia bado iliganda kichwani kwake.Baada ya kuingia ndani moja kwa moja Mathew alielekea katika chumba alimo Jombaa.Tayari Dkt Linus alikwisha rejea na Jombaa alikuwa ametundikiwa chupa ya damu.

“Vipi maendeleo yake? Aliuliza Mathew

“Maendeleo yake ni mazuri” alijibu Dkt Linus

“Unadhani itachukua muda gani kuzinduka? Aliuliza Mathew.Dkt Linus alitazama saa yake akasema

“Nadhani baada ya dakika thelathini hadi arobaini atazinduka”

“Ahsante sana Dkt Linus kwa msaada wako.Pesa yako yote itatumwa katika akaunti yako”

“Usijali ndugu yangu.Ninyi ni watu muhimu sana kwa

taifa hili.Nimefurahi kufanya nawe kazi.” Alijibu Dkt Linus na Mathew akatoka ndani ya kile chumba akarejea sebuleni.Alimsimulia Ruby kile kilichotokea nyumbani kwa Regina.

“Mathew nimeanza kuogopa.Hili suala kumbe ni kubwa kiasi hiki.Hawa jamaa wanaonekana ni mtandao mkubwa.” Alisema Ruby

“Hata mimi sikufikiri kama suala hili linaweza kuwa kubwa kiasi hiki lakini kadriri tunavyozidi kwenda nalo

ndvyo linavyozidi kuwa kubwa.Hawa jamaa wamedhamiria kwa namna yoyote ile kumuua Regina.Baada ya kumkosa kule hotelini waliamini lazima atakwenda nyumbani kwake hivyo wakatuma watu ambao walimkosa wakaua walinzi lakini hawakuondoka walibaki maeneo ya karibu wakiamini lazima Regina angerejea nyumbani kwake.Ilikuwa bahati niliweza kuwabaini haraka nikamuokoa” alisema Mathew

Kilipita kimya kifupi halafu Mathew akasema

“Tukio la usiku huu ni ishara ya wazi kwamba ipo sababu kubwa ya kutaka kumuua Regina.Lazima anaifahamu sababu hiyo na lazima atueleze ili tuweze kumsaidia.Hatuna muda wa kusubiri mlete hapa nje atueleze sababu kwa nini wanataka kumuua?

“Mathew ulidhamiria kweli kumrejesha Regina nyumbani kwake au ulikuwa unamtania tu kuona kama

angeogopa na kutueleza kile tunachokitaka? Ruby aliuliza

“Sikuwa natania.Nilimaanisha.Sitaki kupoteza muda kumbembelea mtu atueleze kitu ambacho ni kwa manufaa yake yeye mwenyewe.Naamini tayari ameiona hatari inayomkabili na atakuwa tayari kutoa ushirikiano” alisema Mathew

“Ninamonea huruma sana” alisema Ruby

“Nenda kamlete tafadhali.”

Ruby alikwenda kumleta Regina kama alivyoelekeza Mathew.

"Regina naamini sasa umeamini kile nilichokuwa nakwambia kwamba uko katika hatari kubwa ya kuuawa.Hawa jamaa wanaokutafuta hawatalala hadi wahakikishe wameondoa uhai wako.Wewe ni mtu hatari kwao ndiyo maana wanafanya kila wawezalo kuhakikisha wanakumaliza tena haraka sana.Tukio la usiku huu limethibitisha hilo.Kama nisingekuwa karibu tayari

ungekwisha uawa.Ninakupa nafasi nyingine ya kutueleza kwa nini hawa jamaa wanakutafuta kwa udi na uvumba wakuue? Wamewekeza fedha na nguvu kuhakikisha wanakumaliza.Why? aliuliza Mathew.

Regina alifuta machozi akasema

“Nisameheni sana kwa kutoshirikiana nanyi wakati ule.Sintafanya hivyo tena.Nitawaeleza kile ambacho naamini ni sababu ya mimi

kutakiwa kuuawa.Lakini kabla ya yote nataka nikushukuru sana kaka yangu kwa kuniokoa.Bila wewe wale jamaa wangeniua.Mpaka sasa bado siamini kama niko mzima” alisema Regina na kufuta machozi.

“Vuta pumzi ndefu halafu tulia na utueleze kila kitu” alisema Mathew.

“Kwanza ni kuhusiana na zile picha mlizozikuta kwa yule jamaa ambaye mnahisi alitumwa na Gavana.Kuna uwezekano mkubwa yule

jamaa kweli alitumwa na Gavana kunichunguza.Nitawaambia kwa nini” alisema Regina akanyamaza kwa muda

“Mwaka mmoja sasa umepita tangu alipotoweka Kelvin Jackson Mzumile mtoto wa kwanza wa Gavana wa benki kuu.” Alisema Regina na kunyamaza

“Kelvin alikuwa mpenzi wangu na tulikuwa katika maandalizi ili anivalishe pete ya uchumba.Kwa bahati mbaya jambo hilo

halikufanikiwa na akatoweka hadi leo hii hakuna anayefahamu kama ni mzima au amefariki” alinyamaza tena kwa sekunde kadhaa

“Niliwahi kulisikia tukio hilo.Unaweza ukatueleza mazingira ya kutoweka kwake? Aliuliza Mathew.Regina alifuta machozi akandelea

“Ilikuwa siku ya jumamosi,Kelvin aliamua kwenda kupunga upepo katika hoteli ya kitalii ya Ansulim iliyoko kandoni mwa bahari.Alipenda sana kwenda

mahali hapo kuogelea na kupunga upepo kutokana na kuwa na ufukwe mzuri na msafi.Siku hiyo tulipanga kuonana jioni aliniambia kuna suala muhimu sana anataka kuniambia hivyo aliniahidi kuwa atanipigia simu kunijulisha ni wapi tutakutana kwa chakula cha usiku" alinyama

"Jioni nikiwa katika maandalizi huku nikisubiri simu ya Kelvin kunielekeza ni wapi tukutane,nilipigiwa simu na namba nisiyoifahamu,nilipoipokea

mpigaji alijitambulisha kuwa ni baba yake Kelvin.Alihitaji kuonana nami.Nilimuelekeza mahali ninakoishi na baada ya muda mfupi akafika.Gavana wa benki kuu Jackson Mzumile alikuwa ameongozana na watu wengine sita.Nilishtuka mno kumuona baba yake Kelvin mahali pale.Kelvin hakuwahi kunitambulisha kwake hata mara moja na alikuwa katika taratibu za kunitambulisha ndipo alipofikwa  na masahibu yale.Gavana alinihoji kuhusu mahusiano yangu na

Kelvin.Nilimueleza ukweli bila kumficha.Baada ya mahojiano yale,aliniuliza kama jioni ile niliwasiliana na Kelvin nikamjibu kuwa niliwasiliana naye saa saba mchana akaniambia bado yupo Ansulim beach hotel akipunga upepo.Gavana alinieleza ukweli kuwa Kelvin ametoweka tangu mchana na hajulikani alipo ndiyo maana amekuja pale kwangu kunihoji.Nilipoteza fahamu baada ya kupewa taarifa ile."
Alinyamaza akafuta machozi

“Nilipozinduka nilitaka kufahamu ukweli kuhusu kupotea kwa Kelvin nikaambiwa kwamba Kelvin aliingia majini akiwa na piki piki ya majini.Alifanya mizunguko kadhaa karibu na ufukwe halafu aliendа mbali zaidi.Baada ya saa moja wavuvi waliokuwa wanaendelea na shughuli zao za kutafuta samaki waliiona piki piki hiyo ikielea majini bila kuwa na mtu ndipo walipotoa taarifa katika hoteli za karibu na ikagundulika piki piki ile ni mali ya  Ansulim

hotel.Walianza kumsaka mtu aliyekuwa anaiendesha ambaye ni Kelvin.Msako wa saa mbili haukuzaa matunda ndipo walipowajulisha jeshi la polisi ambao walifika mara moja na msako ukaendelea bila mafanikio ndipo walipompigia simu Gavana kumfahamisha kile kilichotokea.Gavana alifika eneo la tukio.Ndani ya gari la Kelvin walikuta kila kitu chake pamoja na simu.Walipoichunguza simu ile waligundua kuwa mimi ndiye niliyekuwa mtu wa

mwisho kuzungumza na Kelvin,ndipo aliponipigia simu kutaka kuonana nami. Nililia sana" Regina alinyamaza

Kelvin alitafutwa kwa siku saba bila mafanikio.Nilikuwa mmoja wa watu waliolisaidia jeshi la polisi katika kujua chanzo cha kutoweka kwake.Msako uliendelea kwa miezi sita bila mafanikio ndipo familia yake walipoamini mtoto wao amefariki dunia.Japo jeshi la polisi waliniachia baada ya kuridhika kuwa sihusiki na tukio lile la kutoweka Kelvin,bado Gavana

anaamini kuna kitu ninakifahamu kuhusu kupotea kwa mwanae ndiyo maana amemtuma yule jamaa kunichunguza.Naamini yule mtu alikuwa mpelelezi.” alisema Regina.Kilipita kimya kifupi

“Pole sana Regina kwa masahibu hayo yaliyokupata.Tunalifahamu tukio lile la kutoweka kwa Kelvin kwani liliteka vyombo vya habari.Hata hivyo ninakubaliana nawe kuwa yule mtu Anganile bandia alikuwa mpelelezi ndiyo maana

alikuwa anakufuatilia kila unachokifanya hadi watu unaowakutana nao.Pamoja na hayo nina swali kwa nini Gavana aendelee kuamimi kuwa unafahamu kitu kuhusu kutoweka kwa mwanae? Jeshi la polisi waliridhika kuwa hauhusiki na tukio lile kwa nini Gavana atumie fedha nyingi kukufuatilia hadi akaamua kumuweka mpelelezi? Mathew aliuliza

"Sijui kwa nini anafanya hivi lakini sifahamu chochote kuhusu tukio la kutoweka kwa mwanae." Alisema Regina

“Nini mtazamo wako katika tukio hilo? Aliuliza Ruby

“Tukio lipi? Aliuliza Regina

“Hilo la kutoweka kiajabu kwa Kelvin”

“Mpaka leo ni tukio ambalo linaniumiza sana kwa sababu mimi ndiye niliyekuwa mtu wa mwisho kuzungumza naye ni kama vile tulikuwa tunaagana”

“Unahisi ameuawa? Mathew aliuliza

“Sina uhakika kwa kuwa mpaka leo hii mwili wake haujawahi kupatikana” alijibu Regina

“Utajibu nini mtu akikwambia kuwa Kelvin yuko hai? Aliuliza Mathew.Ilimchukua Regina zaidi ya dakika moja kujibu

“Hilo hal….hakuna anay…oh my Gosh sijui niseme nini lakini sina uhakika kama anaweza kuwa hai”

“Nini kinakufanya uamini amekufa wakati mwili wake

haujapatikana hadi leo hii? Aliuliza

“Mazingira ya kupotea kwake yananifanya niamini lazima alizama majini” alijibu Regina

“Umesema Kelvin alikuwa anafika mara kwa mara hapo hotelini hii ina maana alifahamu kuogelea” alisema Ruby

“Ndiyo alifahamu kuogelea na ndiye aliyenifundisha hata mimi” alisema Regina

“Regina ahsante kwa kutueleza ukweli na sasa tumepata picha kuwa yule Anganile bandia alitumwa na Gavana kukuchunguza.Huo ni upande mmoja, sasa tuhamie katika huu upande unaotaka kukuua.Nashawishika kuamini hizi ni pande mbili tofauti kwa sababu wakati Gavana anakuchunguza kila ukifanyacho akiamini kuna kitu unakifahamu kuhusu kupotea kwa mwanae Kelvin,upande wa pili wao wanataka kukuua kwa gharama zozote.Tena si wewe

peke yako bali na Amani.Why? aliuliza Mathew

“Lazima iwepo sababu kubwa kwa nini watu hawa wanataka kukuua kwa sababu yule mwenzetu mbaye aliletwa kuja kukuua alitengenezewa mtego mkubwa ambao naamini uligharimu fedha nyingi ndipo alipokubali kuja kuifanya kazi hii.Ipo sababu kubwa kwa watu hawa kutumia fedha nyingi kufanikisha kifo chako.Tueleze tafadhali” aliongeza Ruby

Ilimchukua Regina zaidi ya dakika mbili kuinua kichwa na kusema

“Naamini ni chama ndio wanaotaka kuniua”

Mathew na Ruby walitazamana.

“Una maanisha nini Regina? Aliuliza Mathew

“Namaanisha chama changu ndio wanaotaka kuniua”alirudia Regina

“Unaweza ukatueleza kwa nini watake kukuua? Wewe ni kiongozi ndani ya chama ni

naibu katibu mkuu kwa nini wakuue tena wakati kama huu ambao mnaelekea katika uchaguzi mkuu?aliuliza Mathew.Kilipita kimya cha sekunde chache halafu Regina akiwa ameinamisha kichwa halafu akawatazama akina Mathew na kusema.

“Wanataka kuniua kwa sababu wana hofu kubwa na mimi baada ya kuifahamu mipango yangu” alisema Regina

“Mipango ipi Regina? Chama cha ukombozi wa

Afrika ni chama kikubwa kwa nini wakuhofie wewe? Aliuliza Mathew

“Ni kwa sababu nina mpango wa kuhama chama kuhamia katika chama tawala.Wanahofu nikihamia huko basi siri zao zitavuja ndiyo maana wanataka kuniua kabla sijfanikisha mipango yangu” alisema Regina

“Kwa nini unataka kukihama chama chako?

“Nimeamua tu kuondoka ndani ya kile chama baada ya kuona kuna mambo

yanafanyika ambayo binafsi hayajanifurahisha” alijibu Regina

“Regina hebu tuweke wazi katika suala hilo la kuhama chama.Kwa nini wakuue kwa kuhama chama? Una haki ya kuhama chama na kuhamia chama chochote ukitakacho na wewe si wa kwanza,wamekwisha hama chama viongozi wengi tu tena wazito kutoka chama kimoja wakahamia chama kingine.Iweje wewe utakiwe kuuawa kwa kukusudia

kuhama chama? Aliuliza Mathew

“Ni kwa sababu ninazifahamu siri zao.Wana hofu kubwa kama nikihamia katika chama kinachotawala basi nitazianika siri zao.Hawataki hilo litokee ndiyo maana wanataka wanimalize kabla sijafanikisha mpango wangu” alijibu Regina

“Una uhakika gani kuwa ni chama chako ndio wanaokutafuta wakuue? Ruby aliuliza

“Kama nilivyowaambia kuwa wana hofu na mimi baada ya kunasa mpango wangu wa siri wa kutaka kuhama chama.” Alijibu Regina

“Kuna mtu yeyote wa chama chako ambaye umewahi kumshirikisha suala hilo la kuhama chama? Aliuliza Mathew

“Hapana sijawahi kumshirikisha mtu yeyote yule.Mazungumzo yangu na viongozi wa ngazi za juu wa

chama tawala ni ya siri kubwa.”

“Kuhama chama ni jambo ulililoliamua wewe mwenyewe au ulishawishiwa na hao viongozi wa chama tawala? Aliuliza Mathew

“Hakuna aliyenishawishi.Niliamua mimi mwenyewe kwa hiari yangu” Regina alijibu

“Unadhani chama chako wamewezaje kugundua mipango yako ya kuhama chama? Aliuliza Mathew.

“Mpaka sasa sifahamu wamewezaje kugundua lakini naamini ni wao ndio wanaotaka kuniua.Sina ugomvi na mtu yeyote mwingine” alijibu Regina

“Ulituambia kwamba wanataka kukuua kwa sababu kuna siri za chama unazifahamu na ambazo wanahofia endapo utahama chama zinaweza kuvuja.Unaweza ukatuambia ni siri zipi hizo? Aliuliza Mathew.Ilimchukua Regina zaidi ya dakika mbili kutafakari kisha akasema

“Mwaka jana katibu wetu mkuu aliumwa hivyo akalazimika kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu.Mimi ndiye niliyeshika nafasi yake kwa muda wa miezi sita hadi aliporejea.Katika kipindi hicho ndipo nilipoweza kufahamu siri kubwa za chama.” Alinyamaza tena

“Tuambie tafadhali ni siri zipi hizo? Tuamini” alisema Mathew

“Kwanza niligundua kuna mtu anaitwa mfadhili mkuu wa chama ambaye

wanayemfahamu ni watu watatu tu,mwenyekiti,katibu mkuu na mtunza fedha.Hakuna mtu mwingine anayemfahamu huyo mfadhili.Siri iliyopo hapa ni kuwa huyo mfadhili ambaye yuko nje ya nchi ndiye mwenye chama” alinyamaza na kuwatazama akina Mathew baada ya kuonesha mshangao

“Mwenye chama? Una maanisha nini unaposema hivyo? Aliuliza Mathew

“Huyo mtu ndiye mwenye maamuzi ya mwisho katika

hiki chama.Yeye ndiye mwenye kuamua nini kifanyike nini kisifanyike.Yeye ndiye anayetoa fedha zote za kuendesha chama.Hii ni siri inayolindwa sana isijulikane na ukiifahamu lazima wakuondoe.Mfadhili huyo ambaye hata mimi sijafanikiwa hata kulifahamu jina lake ni mmoja wa wawekezaji wakubwa hapa nchini japo sijafahamu anamiliki biashara zipi.Kupitia biashara zake anazomiliki hapa nchini ndipo hupitishia fedha kwenda kwa chama.Hili ni jambo la siri

sana na kama nilivyowaambia wanaolifahamu ni watu watatu pekee.Wakati nikikaimu ofisi ya katibu mkuu,ndipo nilipoibaini hii siri ya kuwepo mfadhili.Nilipojaribu kuuliza niliambiwa nifunge mdomo wangu.Nikithubutu kusema chochote kuhusu jambo hilo utakuwa ni mwisho wangu.Nilipewa kifunga mdomo cha milioni mia moja.Baada ya hapo sikutakiwa tena kuingia katika ofisi ya katibu mkuu kwa kuhofia pengine ningeweza kugundua siri nyingi zaidi”

Regina alinyamaza kidogo halafu akaendelea

“Hilo la kubaini uwepo wa mfadhili wa chama,kwangu lilikuwa suala dogo na lilimalizika japo nilibaki na maswali mengi kichwani ila sikujisumbua kutaka kuhoji au kuchimba zaidi kuhusu huyo mfadhili kwa sababu tayari nilikwisha onywa.Lipo jambo ambalo lilinifanya nitake kuhama chama ambalo ni kubwa zaidi” alinyamaza tena kidogo akafikiri halafu akasema

“Upo mpango kabambe wa kuvuruga uchaguzi mkuu.” Alinyamaza

Ulipita muda wa sekunde kadhaa halafu Mathew akauliza

“Nani wanaotaka kuvuruga uchaguzi mkuu?Mathew aliuliza

“Ipo mipango ya kuhakikisha kwa namna yoyote ile mgombea wa chama cha ukombozi  wa Afrika anashinda uchaguzi mkuu.” Alisema Regina

“Mipango ya ushindi kila chama kinayo.Kila chama kinapoingia katika uchaguzi mkuu lengo lake ni kushinda uchaguzi hivyo mikakati ya ushindi lazima iwekwe.Chama cha ukombozi wa Afrika ni miongoni mwa vyama vikubwa vinne vya siasa hapa nchini na kina wanachama wengi pia.Ni mkakati gani ambao unadhani unaweza kuvuruga uchaguzi mkuu? Aliuliza Mathew

“Ni kweli tunayo mikakati ya kushinda uchaguzi lakini lazima nikiri kuwa uchaguzi huu ni mgumu na hatuwezi

kushinda.Kwanza hatuna idadi kubwa ya wanachama wa kutuwezesha kushinda uchaguzi.Tathmini tuliyoifanya inatuonesha kuwa tuna idadi kubwa ya mashabiki lakini wanachama hai tulio nao hadi wiki hii ni milioni mbili na laki nne kwa nchi nzima.Hii ni idadi ndogo sana ya wanachama.Kitu cha kwanza cha kujihakikishia kushinda uchaguzi wowote ni idadi kubwa ya wanachama kitu ambacho hatunacho.Hatuwezi kuwategemea mashabiki

ambao wengi si wapigaji kura.Ni kwa sababu hiyo basi upo mpango wa siri wa kuhakikisha mgombea wetu anashinda uchaguzi hata kama hatuna idadi kubwa ya wanachama.” Alisema Regina

“Tunataka kuifahamu mikakati hiyo ni ipi? Aliuliza Mathew

“Ni siri kubwa sana ambayo wanaifahamu viongozi wa juu pekee.”

“Wewe ulifahamuje kama ipo mikakati ya kuvuruga uchaguzi? Aliuliza Mathew

“Nilifuatwa na Amani ambaye ni dereva wa mwenyekiti wa chama akanieleza kuwa amekuwa akimsikia mwenyekiti akizungumza katika simu kuhusiana na mipango ya kuhakikisha mgombea wetu anashinda uchaguzi.Nilimtumia Amani kufuatilia kuhusu mipango hiyo ili tuifahamu kwani ni yeye ambaye yuko na mwenyekiti muda wote na wakati mwingine hadi usiku wa manane.Kwa mujibu wa Amani anadai mwenyekiti

amekuwa akikutana na watu wazito wakiwamo vigogo ndani ya serikali"alisema Regina

"Aliwahi kukutajia majina ya hao vigogo ambao mwenyekiti wenu anakutana nao? Mathew aliuliza

"Amani hakunipa majina ya watu ambao mwenyekiti alikuwa anakutana nao kwa sababu muda mwingi tulikuwa tunazungumza katika simu hivyo aliniahidi kunieleza kila kitu pale tutakapokutana ana kwa ana.Leo ndiyo siku ambayo alipanga kunieleza

kila kitu ndiyo maana aliomba apumzike akidai hajisikii vyema.Tulipanga kukutana pale Duma Bar ili twende mahali ambako angenieleza siri zote alizozikusanya.Kwa bahati mbaya hilo halikutokea na Amani amekufa na siri zake.” Alishindwa kuvumilia akaanza kulia.

“Maelezo haya yanatupa picha kuwa hawa jamaa walikuwa wanawafuatilia mazungumzo yenu ya simu ndiyo maana walifahamu hadi mahali mtakapokutana na

wakapanga kuwaondoeni nyote.Hawakutaka katu uzifahamu siri zao ndiyo maana ilikuwa lazima muuawe leo.Pole sana Regina" alisema Mathew

"Nilichelewa kuondoka ndani ya chama nikimsubiri Amani amalize uchunguzi wake.Nilitaka nikishaipata siri hiyo ndipo niondoke chamani lakini sasa kila kitu kimeharibika.Ni mimi ndiye niliyesababisha kifo cha Amani kama si mimi kumtaka kufanya uchunguzi wa siri kuhusiana na mipango miovu

ya chama Amani asingeuawa” alisema Regina na kuinamisha kichwa

“Amani hakuwahi kukudokeza hata kidogo kuhusiana na mipango inayopangwa? Aliuliza Mathew

“Hapana hakunieleza chochote.Leo tulipanga anieleze kila kitu alichokikusanya.Mnaniamini ndugu zangu? Aliuliza Regina

“Tunakuamini Regina.Imekuwa bahati mbaya sana Amani ameondoka na siri zake.Hata hivyo napenda

kukuweka wazi kuwa mambo hayajaishia kwa kumuua Amani.Tayari wamekwisha fahamu wewe ni msaliti.Umezifahamu siri zao hivyo wewe ni mtu hatari sana kwao na kwa gharama zozote zile lazima wahakikishe wanakusaka kokote uliko ili wakuue.” Alisema Mathew

“Nitafanya nini mimi jamani? Nitakimbilia wapi? Aliuliza Regina huku machozi yakiendelea kumtiririka.

“Tutakuwa nawe.Tutakulinda na

kuhakikisha unakuwa salama.Ninachotaka kufahamu ni je hao viongozi wa chama unachotaka kuhamia umekwisha wajulisha chochote kuhusiana na mipango ya chama chako? Aliuliza Mathew

“Hapana sijawaeleza chochote bado japo niliwaahidi kuwa nitakwenda na bomu kubwa.”alijibu Regina

“Mpenzi wako anafahamu kuhusu jambo hili? aliuliza Ruby

“Niliwahi kumdokeza wakati Fulani juu ya mipango

yangu ya kuhama chama.Niliwahi kumdokeza vile vile kuhusu mipango ya chama changu” alisema Regina.

“Kuna siri nyingine yoyote uliyoifahamu kuhusu chama chako? Aliuliza Mathew

“Yapo mambo mbali mbali lakini makubwa ni hayo niliyowaeleza.” Alijibu Regina

“Regina ahsante kwa hayo uliyotueleza.Kwa sasa nakuomba ukapumzike,tupe muda wa kutafakari nini cha kufanya.” alisema Mathew

“Ndugu zangu ninaomba sana mnisaidie niweze kuwasiliana na mume wangu.Yeye anaweza akanisaidia kwani ana undugu na kigogo mmoja mkubwa serikalini” alisema Regina

“Regina kwa sasa naomba ukapumzike.Hutakiwi kuwasiliana na mtu yeyote yule hasa wale wa karibu.Hawa jamaa wanakufuatilia sana hivyo ukijaribu kupiga simu watafahamu mara moja mahali ulipo na hii inaweza ikakuweka katika matatizo

makubwa.Tuamini utakuwa salama" alisema Mathew

Ruby alimchukua Regina akampeleka katika chumba akamtaka apumzike yeye akarudi kuungana na Mathew

"Mwili mzima unasisimka" alisema Ruby

"Jambo hili halijanishangaza hata kidogo.Sijashangaa kwa sababu Tanzania ni nchi tajiri yenye kumezewa mate na mabeberu kila uchao hivyo basi mipango ya kila aina ya kuingia nchini kuvuna utajiri

wetu inafanywa.Kipindi hiki cha uchaguzi ni kipindi muhimu mno kwao kwa sababu lazima wajitahidi kuhakikisha mtu wao anashinda uchaguzi.Kama mipango ya kumuweka madarakni mtu wao ambaye atawasaidia kuchuma mali zetu kushindikana,lazima wahamie katika mpango mwingine ambao ni kuwachonganisha watanzania wafarake,wagombane wenyewe kwa wenyewe hivyo kuwapa mwanya wa kupenya na kuingia nchini.Wakati

tukipigana wao watakuwa wakichota utajiri wetu.Haya mambo yanatokea sana dunia na hasa katika bara la Afrika.Ukichunguza kwa undani migogoro mingi inayotokea katika bara la Afrika utagundua kuna mkono wa mabeberu.” Alinyamaza kidogo Mathew halafu akaendelea

“Kwa bahati mbaya hawa mabeberu hawaji wenyewe,wanawatumia wazawa wa nchi husika.Hutafuta watu wachache wakawapa au

wakawaahidi utajiri mkubwa ili wafanikishe mipango yao.Hawa watu ni  wanyama kabisa kwa sababu hawaangalii athari zinazoweza kutokea, wao wanachohitaji ni mipango yao kufanikiwa.Ninawafananisha watu hawa na walina asali.wanapokwenda msituni kutafuta asali huwasha moto ili kuwatawanya nyuki na hawajali kabisa kama Nyuki wengine watakufa.Wao wanachokihitaji ni kupata asali kwa gharama zozote zile.Tanzania yetu ni mzinga

wenye asali hivyo basi wale wenye kuitafuta asali watafanya kila wawezalo waweze kuipata asali hiyo.Ninamhukuru sana Regina kwa kugundua siri za chama chake.Vyama vya namna hii vipo vingi tu ambavyo vinakuwa na angenda za siri.Ametuambia kuna mtu anaitwa mfadhili ambaye hajulikani ni nani ila ndiye mwenye chama.Ametueleza pia kuwa huyo mfadhili ni mmoja wa wawekezaji wakubwa hapa nchini.Tuna kazi kubwa ya

kuchunguza kuhakikisha tunamfahamu huyo mfadhili ni nani na vile vile kuifahamu mipango yao” alinyamaza Mathew baada ya Dkt Linus kuingia

“Karibu Dkt Linus.Kuna tatizo lolote? Aliuliza Mathew

“Yule jamaa amezinduka.” Alijibu Dkt Linus

“Ahsante sana Dkt LInus.Ninaweza kuzungumza naye? Aliuliza Mathew

“Ndiyo unaweza kuzungumza naye” alijibu Dkt Linus

Mathew na Ruby waliingia katika chumba alimo Jombaa.Aliinua kichwa akamtazama Mathew.

“Jombaa nadhani tayari unafahamu kile kinachoendelea.Hapa si hospitali,hapa si maskani B wala siyo polisi.Tunafahamu wewe ni jambazi sugu na jeshi la polisi wanakutafuta sana wewe na mtandao wako wote wa ujambazi.Sisi

hatutakukabidhi kwa jeshi la polisi.Tutamalizana nawe hapa hapa.Kama tukishindwa kuelewana nawe basi usiku huu utakuwa wa mwisho kwako.Hautatoka humu ndani salama.Wewe ni muuaji lakini nawe leo hii umekutana na wauaji” alisema Mathew.Jombaa aliyekuwa amegeuza kichwa akiwatazama akina Mathew alifumba macho akauma meno kuonesha alikuwa katika maumivu.

“Nini mnakitaka kwangu? Aliuliza Jombaa.Mathew alimsogelea karibu akasema

“Kabla sijakwambia chochote kuna mtu nataka umuone” alisema Mathew akatoka mle ndani baada ya muda akarejea akiwa ameongozana na Regina.Sura ya Jombaa ilionesha mshtuko mkubwa.Hakumuamini kumuona Regina mahali pale.

“Jombaa unamfahamu huyu? Aliuliza Mathew.Jombaa alibaki kimya

“Ni mshangao mkubwa kwako.Hukutegemea kabisa kumuona hapa.Huyu ndiye yule ambaye ulitumwa kwenda

kumuua.Kitu cha kwanza ninachotaka utueleze ni nani aliyekutuma kumuua Regina? Aliuliza Mathew.Jombaa alibaki kimya

“Jombaa najua hukuamua tu wewe mwenyewe kumuua.Wewe ni  mtu wa kutumwa kazi.Tunahitaji kumjua yule aliyekutuma kufanya mauaji hayo” alisema Mathew

“Ninyi ni akina nani? Aliuliza Jombaa

“Jombaa jibu maswali unayoulizwa na si kuanza

kuuliza maswali.Nani aliyekutuma umuue Regina? Aliuliza Mathew.Swali lile lilionekana kuwa gumu kwa Jombaa.Mathew akamtaka Ruby kumrejesha Regina chumbani kwake.

“Sasa tumebaki wawili.Yule mwanamke anaitwa Regina.Ni naibu katibu mkuu wa chama cha siasa cha ukombozi wa Afrika.Nataka uniambie nani aliyekutuma kumuua? Aliuliza Mathew.Bado Jombaa hakuwa tayari kujibu.

“Jombaa sitaki kutumia nguvu kukulazimisha ujibu maswali yangu ila pale itakaponilazimu kufanya hivyo basi nitatumia nguvu lakini sitaki tufike huko.Sitaki kukuharibia maisha yako,ninachohitaji ni msaada wako.Siku mbili zilizopita ulimpokea mtu mmoja anaitwa Gosu Gosu ukaishi naye katika makazi yako.Huyu ndiye aliyeletwa kuja kufanya mauaji lakini maelekezo yote alitakiwa kuyapata toka kwako.Kuna mambo mawili ambayo nataka kuyafahamu kutoka

kwako.Kwanza nani aliyekukodisha kufanya mauaji? Pili,yule jamaa aliyeletwa kuja kufanya mauaji yuko wapi? Ukinijibu maswali hayo mawili nakuhakikishia Jombaa utakuwa salama.” Alisema Mathew.Jombaa hakujibu kitu.Alibaki anatazama juu.

“Waliokupa kazi walikulipa kiasi gani? aliuliza Mathew lakini bado Jombaa hakuwa tayari kujibu

“Jombaa nataka kujua kiasi walichokulipa.Mimi

ninataka kukulipa mara mbili au hata tatu ya fedha walizokupa ili uweze kunijibu maswali yangu.Nataka tulimalize suala hili bila kukwaruzana.Niambie tafadhali kiasi gani nikupatie ili unipe majibu ninayoyahitaji? Aliuliza Mathew.Jombaa bado alikuwa kimya

“Jombaa naamini hufanyi haya kwa sababu wewe ni mtu mwenye roho mbaya bali kwa sababu ya pesa.Hakuna anayefurahia kuua au kutoa roho za watu ila tunalazimika

kufanya hivyo kwa ajili ya kujipatia kipato.Mimi nawe tunaweza kuwa marafiki na nikakusaidia sana katika mambo mengi.Kwa mfano hivi sasa tayari jeshi la polisi watakuwa wamefika katika ile maskani yako ambako ilisikika milio ya risasi na wataukuta mwili wa kijana wako Jera katika dimbwi la damu.” Mathew alinyamaza baada ya Jombaa kuonesha mshtuko

“Ndiyo utashangaa lakini Jera hayupo tena duniani.Ameuawa na moja ya silaha zako wewe mwenyewe

hivyo polisi wataanza kukusaka kila kona.Kwa wakati huu ni mimi pekee ambaye ninaweza kuwa na msaada kwako.Ni mimi ninayeweza kukuondoa katika tatizo ulilonalo.Kwa nini tuendelee kuwa maadui wakati tunaweza kusaidiana? Tafadhali niambie ni kiasi gani cha fedha unakihitaji nikupatie uondoke kabisa hapa nchini." Alisema Mathew

Zilipita dakika tatu Jombaa akififikiria halafu akasema

“Nitakwenda wapi wakati tayari nina jeraha la risasi mguuni? Wewe ni mtu mjinga sana” alisema Jombaa

“Jombaa huu si wakati wa kutukanana au kulaumiana.Kama nisingekuwahi lazima ungeniwahi.Tusipoteze muda niambie tafadhali unataka nikulipe kiasi gani kwa ajili ya kununua taarifa ninayoitaka? Aliuliza Mathew

“Kwa nini unataka sana kupata taarifa hiyo? Wewe ni nani kwanza? Aliuliza Jombaa

“Mimi si askari lakini kazi yangu ni kupambana na mitandao ya kihalifu kama hao waliokutuma ufanye mauaji.Tusipoteze muda tafadhali kwa mahojiano.Naomba tafadhali unieleze kuhusu hao watu au niambie nikulipe kiasi gani kwa ajili ya kuniambia watu hao ni akina nani” alisema Mathew

“Nitaaminije kama haya yote uyasemayo ni ya kweli? Aliuliza Jombaa

“Kama hujawahi kumuamini mtu yeyote katika maisha yako naomba leo iwe ni mara ya kwanza kuamini mtu.Ninakwambia kitu cha kweli siwezi kukudanganya.Tumalize hili suala nikuache upumzike” alisema Mathew

“Nikikutazama macho yako pamoja na yule mwenzako nyote wawili mnaonekana ni wauaji.Japokuwa umeniumiza lakini nipe milioni tano tumalize jambo hili” alisema Jombaa

“Milioni tano si kitu.Niambie kuhusu hawa watu tafadhali” alisema Mathew

“Siwezi kusema chochote sasa hivi hadi pale nitakapopopata uhakika wa hiyo hela” alisema Jombaa

“Nitajie namba yako ya akaunti ya benki au simu” alisema Mathew.Jombaa alimtajia namba yake ya akaunti ya benki .Mathew alichukua simu yake akahamisha kiasi cha fedha alichokihitaji Jombaa halafu

akamuonesha ujumbe kuwa fedha aliyoihitaji imekwisha tumwa katika akaunti yake.Jombaa alikohoa halafu akafumba macho kama vile anaugulia maumivu halafu akasema

“Sijawahi kukutana na watu hao ana kwa ana na wala siwafahamu.Nilifuatwa na mtu mmoja anaitwa Kinje ambaye ni muuzaji magari hapa jijini Arusha.Aliniambia kuna mtu anahitaji kufanyiwa kazi yake.Mimi sichagui kazi hivyo nilimtaka aniunganishe na huyo mtu.Nilimpa namba

yangu ya simu na siku iliyofuata nilipigiwa simu na mwanamke mmoja akaniambia kuwa ni yeye aliyemtuma Kinje.Aliniuliza kama ninaweza kuifanya kazi yake nikamuuliza ni kazi gani akaniambia kuna watu watatu ambao anataka wauawe.Aliniweka wazi kuwa kazi yangu itakuwa ni kufanya maandalizi ya kuwaua watu hao lakini atakayefanya mauaji hayo ni mtu mwingine.Nilikubali na usiku wa siku hiyo alinitumia shilingi milioni mbili

akaniambia kazi itakapokamilika atanimalizia milioni tatu.Siku iliyofuata alikuja mtu kutoka Dar es salaam akanionesha picha ya mtu wa kwanza ambaye anatakiwa kuuawa.Niliambiwa mtu huyo anaishi katika hoteli moja hapa nchini na kazi yetu ni kumchunguza nyendo zake zote.Tulifanya hivyo na kumpa majibu.Baada ya siku tatu alileta yule mtu maalum kwa ajili ya mauaji.Yule jamaa aliifanya kazi yake vizuri.Baada ya kumuua yule mtu nilipewa maelekezo ya

kuhusiana na kazi ya pili ambayo ni kuwaua wale watu wawili.Jioni ya leo nilipewa maelekezo ya kwenda Duma bar ambako ndiko mauaji yangefanyika.Nilikutana na hao watu kwa mara ya kwanza nikaoneshwa watu wanaotakiwa kuuawa.Alifanikiwa kuuawa mmoja lakini yule mwanamke alinusurika.Hivyo ndivyo ilivyokuwa.” Alisema Jombaa

“Yule jamaa aliyeletwa kuja kufanya mauaji hayo yuko wapi? Aliuliza Mathew

“Kuna jambo lilitokea wakati wa kutekeleza mauaji yale ambalo halikuwafurahisha wale jamaa.Wanahisi alifanya makusudi .Alipigwa na chuma akapoteza fahamu kisha jamaa wakaondoka naye.”

“Walielekea wapi? Mathew aliuliza

“Sifahamu walikoelekea.Nililipwa fedha zangu nikaachana nao” alijibu Jombaa

“Unadhani kwa nini alileletwa yule jamaa kuja kuifanya kazi hiyo wakati ninyi

mngeweza kuifanya? Aliuliza Mathew

“Hayo ni matakwa ya mwenye kazi.Mimi nilipewa jukumu la kufanya nikalitekeleza nikalipwa changu sitaki kujua kwa nini aliletwa yule jamaa kuja kufanya mauji yale” alijibu Jombaa

“Watu hao uliokutana nao pale Duma bar umewahi kukutana nao hapo kabla? Mathew aliuliza

“Hapana.Watu wale ni mara ya kwanza kukutana

nao.Wanaonekana ni wataalamu wa kompyuta kwa sababu ndani ya kile chumba kulikuwa na kompyuta kadhaa halafu wale jamaa wenyewe hawakuonekana kama ni watanzania kwa sababu hawakuwa wanazungumza Kiswahili.Ni mmoja tu ndiye aliyekuwa anazungumza nami Kiswahili.”

“Kompyuta hizo zilikuwa za kazi gani? Unahisi hao watu walikuwa wanawafuatilia wale watu waliotakiwa kuuawa? Aliuliza Mathew

“Ni kweli walikuwa wanawafuatilia kwa sababu mara tulipoingia ndani ya kile chumba nilioneshwa kupitia kompyuta watu wanaotakiwa kuuawa.Walikuwa wameketi katika meza wakipata kinywaji.Sifahamu waliwezaje kupata picha zao” alisema Jombaa

“Rafiki yako Kinje aliyekuunganisha na huyo mwanamama aliyekupa kazi,unahisi ana mahusiano na hao watu uliowakuta ndani ya hicho chumba? Aliuliza Mathew

“Sina hakika kama anawafahamu wale watu”Alijibu Jombaa halafu kikapita kimya kifupi

“Kitu gani kingine unahitaji kukifahamu? Aliuliza Jombaa

“Kwa sasa niliyohitaji kuyafahamu ni hayo.Endelea kupumzika nitakuja tena kwako baadae” alisema Mathew na kutoka mle chumbani akamfuata Ruby aliyekuwa sebuleni akicheza na kompyuta yake.

“Amefunguka Jombaa? Aliuliza Ruby

“Ndiyo amefunguka” alijibu Mathew na kumweleza Ruby kile alichokisema Jombaa

“Unaamini anasema ukweli? Aliuliza Ruby

“Ndiyo anasema ukweli” alijibu Mathew.Ruby aliiweka mikono yake kichwani akaegemea sofa.

“Nimechanganyikiwa.Tuta mpata wapi Gosu Gosu?Hawa jamaa hawatamuua? Aliuliza

Ruby.Sebule ilikuwa kimya hadi waliposhtuliwa na Dkt Linus ambaye aliingia akitokea nje alikokuwa anavuta sigara.Hakuwasumbua akina Mathew moja kwa moaja akaelekea katika chumba alimo mgonjwa wake.

“Kitu cha kwanza kabla ya kushughulikia kile alichokisema Regina ni kuhakikisha Gosu Gosu amepatikana.Sehemu pekee ya kuanzia kumsaka ni kwa mama yake Ambola.” Alisema Mathew

“Itatulazimu kurejea Dar es salaam”

“Ndiyo.Itatulazimu kurejea Dar es salaam” alijibu Mathew

“Vipi kuhusu Regina?

“Regina tayari ni mzigo wetu hatuwezi kumuacha hapa Arusha.Lazima tuhakikishe anakuwa salama.Kuwa karibu na Regina ni hatari tupu kwani wale wanaomuwinda ni watu wenye nguvu.Hata hivyo hatupaswi kuogopa.Kutakapopambazuka nitaangalia uwezekano wa

kupata helkopta ya kukodi itakayotuondosha hapa Arusha kurejea Dar es salaam.Hatutaweza kutumia usafiri mwingine kama ndege au basi ili kuzuia Regina asionekane.Wakati tukisubiri mapambazuko lazima tuanze kulichambua hili suala la Regina." Alisema Mathew na kunyamaza kwa muda.

"Kwanza kabisa kuna pande mbili zinazomfuatilia Regina ambazo naamini hazina mahusiano wala mashirikiano.Kwanza ni upande wa Gavana.Huyu

anamchunguza Regina.Sababu kuu tuliyoipata ni kutokana na kutoweka kwa mwanae ambaye alikuwa na mahusiano na Regina.Gavana anaamini kwa asilimia kubwa kuwa Regina kuna kitu anakifahamu au anahusika katika kutoweka kwa mwanae ndiyo maana ameamua kumfuatilia na kumchunguza.Yule mtu aliyeuawa ni nani? Katokea wapi? Kwa nini Gavana aamini kuna kitu Regina anakifahamu kuhusu kupotea kwa mwanae? Je ni kweli Regina kuna kitu anakifahamu kuhusu

kutoweka kwa mtoto wa Gavana? Hayo ni maswali machache ambayo tunapaswa kujiuliza katika upande huo wa kwanza.Sehemu pekee ambayo tunaweza kupata majibu kwa upande huo ni kwa kuonana na Gavana Jackson Mzumile." Alisema Mathew

"Ni namna gani tutaweza kuonana na Gavana Jackson? Ruby aliuliza

"Tutatafuta namna yoyote ile hadi tumpate na kuzungumza naye" alijibu Mathew

“Upande wa pili ni wale wanaotaka kumuua.Kundi hili linaongozwa na mama yake Ambola.Huyu ndiye aliyemtuma Gosu Gosu Arusha kuja kumuua Regina pamoja na yule Anganile bandia.Swali la kwanza la kujiuliza kwa nini Gosu Gosu atumike kufanya mauaji yale? Kwa nini hawakutaka kuwatumia akina Jombaa ? Kwa nini Anganile bandia aliuawa? Walifahamuje kama anamfuatilia Regina? Regina anahisi wanaotaka kumuua ni chama chake baada ya kuzifahamu siri zao.Hata

mimi ninashawishika kuamini hivyo lakini je huyu mama yake Ambola naye ana mahusiano yoyote na chama cha ukombozi wa Afrika? Sehemu ya kuanzia kutafuta majibu ya maswali haya ni kwa mama yake Ambola.Hii ni sababu nyingine ambayo itatulazimu kurejea Dar es salaam ambako huyu mama yupo" alisema Mathew

"Mathew unadhani Regina ametueleza kila kitu kuhusu sababu ya yeye kutakiwa kuuawa? Ruby aliuliza

“Yawezekana kuna mambo anayaficha lakini kwa haya aliyotueleza yanatosha kuanzia uchunguzi wetu.Hata kama bado yapo mengine anayaficha tutaunganisha vipande vya picha tutapata picha kamili.” Alisema Mathew

“Unahisi mume wake anaweza akahusika kwa namna yoyote katika mpango huu wa kumuua Regina?aliuliza Ruby

“Ni mapema sana kusema chochote kwa sasa katika suala hili.Tulifanyie uchunguzi

kwanza na tutafahamu kila anayehusika.Tuna mlima mrefu wa kupanda.Hili jambo ni kubwa linahitaji kushughulikiwa kwa umakini mkubwa.Kwa sasa tuanze kushughulikia namna ya kuondoka mahali hapa kurejea Dar es salaam." Alisema Mathew.

***************

Gari mbili aina ya Landcruiser zenye rangi ya kijani ambazo hutumiwa kwa shughuli za kitalii zilifunguliwa geti kubwa na kuingia katika jengo kubwa lililoonekana kama bohari lililozungushwa na ukuta mkubwa.Kulikuwa na magari mengi mle ndani kuashiria ile ilikuwa ni gereji ya kutengenezea magari.Lango la lile jengo kubwa lilifunguliwa mojawapo ya zile gari mbili likaingia ndani.Haraka haraka mlango ulifunguliwa wakashuka watu

wanne baada ya muda mfupi akashushwa akiwa amefungwa kamba kumzunguka mwili mzima.Kichwani alikuwa amevalishwa mfuko mweusi.Jamaa watatu waliojazia miili yao walijitokeza na kumbeba yule mtu wakamlaza chini.Walijadiliana kwa muda halafu mmoja wa wale jamaa alitoa maelekezo wale jamaa watatu wakambeba yule mtu waliyemlaza chini wakamuingiza katika moja ya chumba kilichokuwa ndani ya lile jengo.Alifunguliwa kamba

alizokuwa amefungwa mwilini halafu akafungwa katika kiti cha chuma.Mfuko aliofungwa kichwani ulitolewa .Yule mtu alikuwa ameinamisha kichwa.Mmoja wa wale jamaa alitoa kitu kidogo mfukoni kama chupa ndogo akamuwekea yule jamaa puani.Baada ya sekunde chache yule jamaa alipiga chafya mfululizo.Aliinua kichwa akazungusha macho ndani ya kile chumba ambacho kilikuwa na vipuri vingi vya magari.Aliwatazama pia wale

watu waliokuwa ndani ya kile chumba.

“Kwa nini mnanifanyia hivi? Alifoka yule jamaa lakini hakuna aliyemjibu.

Mmoja wa wale watu aliwasiliana na mtu katika simu halafu alichukua kiti akaketi karibu na yule mtu aliyefungwa katika kiti cha chuma.Alimtazama kwa makini sana akasema

“Kwa nini umeharibu kazi? Kwa nini umekwenda kinyume na maelekezo uliyopewa? Alifoka yule jamaa.

“Sijaharibu kazi.Nimefanya kazi yenu kama nilivyoelekezwa.” Alijibu yule jamaa aliyefungwa kitini

“Kazi umeiharibu makusudi kabisa.Hukutaka kumuua yule mwanamke.Kwa nini? Aliuliza yule jamaa.Yule jamaa aliyefungwa katika kiti alimtazama kwa dharau yule mtu aliyekuwa anamuuliza maswali halafu akasema

“Sikukubaliana na kiongozi wenu kama nitaua watu wawili leo.Makubaliano yetu yalikuwa kuua mtu

mmoja na nimefanya hivyo.Wale wengine hawakunihusu ndiyo maana nilijielekeza kwa mtu yule mmoja” alijibu kwa dharau.

“Ahsante kwa jibu hilo.Sasa tumejua ulifanya makusudi kabisa kuharibu kazi.Tunataka jibu kwa nini uliharibu kazi? Aliuliza yule jamaa.

“Mnafanya kosa kubwa sana kuvunja makubaliano yetu.Nilikubaliana na kiongozi wenu kuifanya kazi yake lakini hata baada ya kuifanya kazi

yake lakini bado mnaendelea kunishikilia.Ninawahakikishia hili ni kosa kubwa mmelifanya.”

“Kauli za vitisho hazitakusaidia.Tunachohitaji ni kujua kwa nini uliharibu kazi? Aliuliza tena yule jamaa lakini hakujibiwa.

“Tutaondoka nawe tutakwenda kuzungumza vizuri mbele ya safari.” Alisema yule jamaa halafu akageuka akampa ishara jamaa mwingine ambaye alifungua sanduku akatoa

sindano akamsogelea yule mtu aliyefungwa katika kiti akamchoma ile sindano shingoni.Baada ya muda mfupi yule jamaa alilegea na kuangushia kichwa kwa mbele.Alifunguliwa kutoka kitini akafungwa kamba kama alivyokuwa amefungwa mwanzo,akavishwa na ule mfuko mweusi kichwani.Waliingia wale jamaa watatu waliojaza miili yao wakambeba na kumtoa nje ya chumba akaingizwa katika gari aina ya Range rover lenye rangi nyeusi wakamlaza

upande wa nyuma.Wale jamaa wanne waliingia katika ile Range rover wakatoka nje ya lile jengo ambako walikuta kuna gari lingine kama lile likiwasubiri.Magari yale mawili yalitoka nje ya ile karakana ya kutengenezea magari safari ikaanza kuelekea kusikojulikana.

***************

Jiji la Arusha liliamshwa na taarifa mbaya za mauaji yaliyotokea ndani ya jiji hilo usiku.Kila mahali mazungumzo makubwa yalikuwa ni mauaji yaliyofanyika baada ya Duma ambako dereva wa mwenyekiti wa chama cha Ukombozi wa Afrika aliuawa kwa kupigwa risasi.

Katika makazi ya muda walikopanga akina Mathew hali ilikuwa shwari.Dkt Linus alilala pale kuhakikisha

mgonjwa anakuwa salama.Hadi mapambazuko hali ya Jombaa ilikuwa nzuri sana.Dkt Linus aliagana na akina Mathew ambao walimshukuru kwa huduma yake na kumtaka atunze siri ya kile kilichofanyika mahali pale usiku.Baada ya Dkt Linus kuondoka Mathew alimfuata Jombaa chumbani akamjulia hali.

“Saa ngapi mtaniacha niende zangu? Nimewaeleza kila mlichotaka kukifahamu” alisema Jombaa mara tu Mathew alipoingia chumbani.

“Daktari ameniambia maendeleo yako ni mazuri lakini siwezi kukuacha ukaondoka sasa hivi hadi hapo tutakapokuwa tumeondoka Arusha.Hii ni kwa ajili ya usalama wako na usalama wetu pia” alisema Mathew

“Naombeni mniache niondoke zangu.Msiwe na hofu na usalama wangu.Arusha ni jiji langu hivyo niko salama.Viongozi wote wa jiji hili wananifahamu na wanaifahamu kazi yangu.Kuhusu ninyi japo mmeua kijana wangu lakini

naheshimu makubaliano yetu sintasema chochote juu yenu” alisema Jombaa.Mathew alimtazama akasema

“Baadae leo tutaondoka .Sikwambii tunakwenda wapi lakini pale tutakapoondoka ndipo utakapobaki huru” alisema Mathew na kunyamaza baada ya Ruby kumletea simu yake.Mathew alitoka ndani ya kile chumba akaipokea.Alizungumza na aliyempigia kwa takribani dakika kumi halafu akamchukua Ruby wakaenda sebuleni.

“Niliyekuwa nazungumza naye anaitwa Peterson ambaye ni mkurugenzi wa kampuni yenye kukodisha helkopta.Ni rafiki yangu na ndiye nilizungumza naye nikamjulisha kuwa ninahitaji kukodi helkopta ije kunichukua Arusha.Hakuweza kunipa jibu usiku ule hadi pale atakapokuwa na uhakika na helkopta iliyopo.Baada ya kupata uhakika ndipo amenijibu lakini anataka helkopta hiyo ikatue aidha katika uwanja wa ndege wa Arusha au

Kilimanjaro.Nimememwambia lazima iwe ni nje ya uwanja wa ndege.Amenipa kazi ya kutafuta mahali ambako ninataka helkopta hiyo ikatue kisha nimjulishe haraka." Alisema Mathew

"Jombaa ni mwenyeji sana wa hapa Arusha anaweza akaifahamu sehemu nzuri ambako helkopta inaweza ikatua" alisema Ruby

"Good idea" alisema Mathew na kupiga hatua kwenda chumbani kwa Jombaa

“Jombaa kuna jambo nahitaji msaada wako.Wewe ni mwenyeji sana wa jiji la Arusha.Unafahamu sehemu yoyote ya wazi isiyo na mkusanyiko wa watu ambako helkopta inaweza ikatua?Ikiwa nje ya jiji itakuwa vizuri sana” alisema Mathew

“Mnaondoka na helkopta? Aliuliza Jombaa

“Ndiyo” alijibu Mathew

“Hilo mbona ni suala dogo sana.Ninaye rafiki yangu ana hoteli kubwa ya kitalii iko Usa river kuna sehemu ya kutua

helkopta.Nipe simu nizungumze naye” alisema Jombaa.Mathew alimpa simu yake akaandika namba ya simu ya huyo rafiki yake akampigia.Simu iliita ikapokelewa.Alizungumza na mtu aliyempigia kwa dakika kadhaa halafu wakaagana akakata simu

“Amekubali.Hoteli inaitwa Sangara Lodge iko nje kidogo ya mji wa Usa river.” Alisema Jombaa

“Ahsante kwa msaada huo.Utaongozana nasi hadi

mahali hapo.Tunalo gari la kukodi ambalo tutakuomba ulirejeshe katika kampuni tuliyolikodi mara baada ya sisi kuondoka.Naamini hilo halitakuwa tatizo kwako" alisema Mathew

"Hilo si tatizo.Nitawasaidia kulirudisha gari hilo.Mimi na ninyi tumekuwa marafiki tayari japo mmenipa hasara kubwa kwa kumuua kijana wangu Jera" alisema Jombaa

"Ile ilikuwa ajali kazini.Utanisamehe kwa hilo."

Alisema Mathew na kutoka nje akaenda kuzungumza na Peterson kumjulisha mahali ambako helkopta inatakiwa kwenda kutua.

“Kwa sasa tuna uhakika wa kuondoka salama hapa Arusha.Wakati tunasubiri helkopta kuna kitu tunatakiwa kukifanya.Regina anatakiwa kupata mavazi ya kujifunika mwili mzima hadi uso ili isiwe rahisi kwa mtu yeyote kumtambua.Jombaa atanielekeza ni wapi ninaweza kupata mavazi hayo nitakwenda mara moja

kununua” alisema Mathew akamfuata Jombaa akamtaka amuelekeze duka ambako angepata mavazi ya wanawake ya kufunika mwili mzima.Baada ya kuelekezwa,Mathew hakupoteza muda aliwasha gari akaelekea mahali alikoelekezwa.

***************

Mathew alirejea katika makazi yao ya muda akiwa na mavazi ya kufunika mwili aliyonunua katika duka aliloelekezwa.Regina alipewa mavazi yale ili ajaribu.Wakati wakisubiri kuona muonekano wa Regina,mara walisikia Jombaa akiita.Wote walikwenda katika chumba chake kujua kile kilichomsibu.

“Kuna nini Jombaa? Aliuliza Mathew

“Tazama katika runinga” alisema Jombaa

Runingani kamanda wa polisi wa mkoa wa Arusha alikuwa anazungumza na wanahabari.

“Kuna matangazo ya moja kwa moja kutoka Arusha.Kamanda wa polisi wa mkoa wa Arusha anazungumza na wanahabari” alisema Jombaa.Mathew na Ruby wote walijielekeza katika runinga.

“Ndugu wanahabari nimewaiteni hapa kuwapeni taarifa kuhusiana na matukio kadhaa ya mauaji yaliyotokea katika jiji letu la

Arusha.”alisema kamanda wa jeshi la polisi Arusha.

“Siku tatu zilizopita aliuawa mtu mmoja katika hoteli ya Kongwa.Mtu huyo ambaye mpaka sasa bado hajatambulika alivamiwa chumbani kwake hotelini hapo na watu wasiojulikana wakamuua.Mpaka sasa mwili wake umehifadhiwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa ya mount Meru.Tunawaomba wale wote ambao wamepotelewa na ndugu yao wajitokeze kuutambua mwili huo.Marehemu hakukutwa na

kitambulisho au kitu chochote cha kumtambulisha yeye ni nani na ametokea wapi.Upelelezi wa tukio hilo bado unaendelea” alisema kamanda wa polisi akanyamaza kidogo

“Usiku wa kuamkia leo kumetokea matukio matatu ya mauaji.Tukio la kwanza lilitokea katika baa ya Duma ambako dereva wa mwenyekiti wa chama cha Ukombozi wa Afrika alipigwa risasi na kuuawa wakati akipata kinywaji na wenzake.Kabla ya kutokea tukio hilo marehemu

alikuwa akipata kinywaji na wenzake ambao kwa mujibu wa mashuhuda ni naibu katibu mkuu wa chama hicho upande wa bara bi Regina William Zanga pamoja na mtu mwingine ambaye hadi sasa hajafahamika ni nani.Wakati wakiendelea kupata kinywaji ilisikika milio miwili ya risasi kutoka katika bastola watu wote wakakimbia.Baada ya watu wote kutawanyika ndipo ilipobainika dereva yule aitwaye Amani alikuwa amepigwa risasi.Askari polisi waliokuwa doria walifika eneo

la tukio kwa haraka sana mara tu walipopata taarifa ya kutokea kwa tukio hilo.Askari wetu walipofika eneo la tukio walikuta tayari Amani amekata roho.Eneo la tukio zilikutwa simu mbili ambazo ni mali ya Regina Zanga.Vile vile iliokotwa bastola ambayo baada ya kuifanyia uchunguzi tumebaini inamilikiwa na Regina Zanga.Bastola hiyo ndiyo inayodaiwa kutumika katika mauaji hayo."

Alinyamaza kidogo akavaa glovu mikononi akawaonesha

waandishi wa habari bastola ile

“Mungu wangu suala hili mbona limekuwa kubwa namna hii ! Alisema Ruby

“Mzigo wa mauaji tayari umemuangukia Regina” alisema Mathew

“Mhh ! Jombaa aliguna

“Ndugu waandishi wa habari” aliendelea kamanda wa polisi

“Askari wetu waliuchukua mwili wa Amani wakaupeleka hospitali ambako madaktari

walithibitisha kuwa tayari amefariki dunia.Usiku huo huo tulianza kumsaka Regina.Jeshi la polisi walifika mahali anakoishi eneo la Ngaramtoni lakini walipofika mahali hapo walikuta mauaji mengine yamefanyika ndani ya nyumba hiyo.Walinzi wawili waliokuwa wakilinda nyumba hiyo walikutwa wameuwa.Pia ulikutwa mwili wa mwanamke mwingine ambaye anadaiwa ni mtumishi wake wa ndani.Mpaka sasa jeshi la polisi linaendelea kumsaka Regina ambaye amekimbia na

hajulikani alipo.Tunawaomba wananchi watoe taarifa kwa jeshi la polisi pale watakapomuona huyu Regina mahali kokote.” Alisema kamanda wa polisi na kuwaonesha waandishi wa habari picha ya Regina

“Tunaomba ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi watuhabarishe popote pale watakapomuona mtuhumiwa huyu.”alisisitiza kamanda wa polisi

“Dah ! alisema Ruby akiwa ameshika kiuno.Alihisi kuishiwa nguvu.

“Nimechanganyikiwa.Siku tegemea kabisa kama suala hili lingekuwa kubwa kiasi hiki” alisema Ruby

“Mambo ndiyo kwanza yameanza.” Alisema Mathew kwa sauti ndogo

“Usiku wa kuamkia leo pia kulifanyika tukio lingine la mauaji katika nyumba moja mtaa wa Msalele. Jeshi la polisi lilipokea taarifa kutoka kwa raia wema katika mtaa wa

Msalele kuhusu kusikika milio ya risasi katika nyumba moja ambayo wamekuwa wakiitilia shaka muda mrefu hasa kutokana na aina ya watu wanaoonekana mara kwa mara katika nyumba hiyo. Jeshi la polisi walifika kwa haraka katika mtaa huo na katika nyumba waliyoelekezwa.Waliingia ndani na kumkuta mtu mmoja akiwa amekwisha fariki dunia kwa kupigwa risasi.Jeshi la polisi lilifanya upekuzi katika nyumba hiyo na walifanikiwa kupata silaha mbali mbali

ambazo zilikuwa katika harakati za kuhamishwa.Silaha zilizokutwa katika nyumba hiyo ni bunduki za kivita nne,bastola saba,mabomu sita ya kurusha kwa mkono,fulana za kujikinga risasi,sare za jeshi la polisi” alisema kamanda wa polisi mkoa wa Arusha kisha akaanza kuwaonesha waandishi wa habari silaha mbali mbali ambazo zilikutwa ndani ya nyumba hiyo.Jombaa alikuwa anatetemeka.Baada ya kuwaonesha waandishi wa habari silaha zile,kamanda wa

jeshi la polisi mkoa wa Arusha akaendelea.

"Jeshi la polisi linamtafuta mtu anaitwa Jonathan Zumba au maarufu kama Jombaa.Huyu ni jambazi sugu hapa Arusha na ndiye mmiliki wa nyumba ambamo yalifanyika hayo mauaji.Jambazi huyu amekuwa akijihusisha na matukio mbali mbali ya kihalifu katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.Jeshi la polisi linaahidi kutoa zawadi nono kwa mtu yeyote atakayetoa taarifa

zitakazowezesha kupatikana kwa jambazi huyu." Alimaliza kamanda wa polisi mkoa wa Arusha kwa kuwaonesha waandishi wa habari picha ya Jombaa.

"Mmeniingiza katika matatizo makubwa ninyi watu.Muda mrefu nimefanya kazi zangu kwa amani bila kuwa na mgogoro na vyombo vya dola lakini mmekuja ninyi mmeyaharibu maisha yangu" alisema Jombaa huku sura yake ikiwa imejikunja kwa hasira.

“Kila jambo lina mwanzo na mwisho wake.Huu ni mwisho wako wa kujihusisha na masuala ya uhalifu.Yawezekana unahitajika kuifanya kazi nyingine.Nitaondoka nawe kwenda Dar es salaam” alisema Mathew

“Dar es salaam? Jombaa alishangaa

“Ndiyo.Ninataka kukusaidia kukuondoa hapa Arusha.Picha yako tayari imesambazwa katika mitandao yote ya kijamii hivyo

hautamaliza siku moja kabla hujakamatwa.Ni juu yako kuamua hatima ya maisha yako.Sikulazimishi lakini ninakushauri kama unataka kuendelea kuwa salama ambatana nasi kwenda Dar es salaam" alisema Mathew halafu akatoka ndani ya kile chumba akamfuata Regina chumbani kwake akamkuta akijiandaa kujaribisha vazi la pili.

"Kwa nini unaingia bila hodi? Ni vipi kama ukinikuta nikiwa mtupu? Aliuliza Regina akionesha kutokufurahishwa

na kitendo cha Mathew kuingia mle ndani bila hodi.

“Utupu wako hauna maana yoyote kwa sasa.Nisikilize vizuri” alisema Mathew

“Mapambano yameanza” alisema Mathew na kumueleza Regina kile walichokishuhudia kikitangazwa katika runinga.Regina alijikuta akiishiwa nguvu akakaa chini.Aliangua kilio kikubwa

“Jamani mimi maisha yangu yameharibika.Nitakwenda

wapi mimi? Nitakuwa mgeni wa nani katika hii dunia? Alisema Regina huku akimwaga machozi.Mathew alimshika mikono akamuinua.

“Hebu sikiliza Regina.Machozi hayatakutoa katika hili tatizo ulilonalo.Nataka uniambie ni kweli ile bastola ambayo inadaiwa kukutwa eneo la tukio ni ya kwako? Aliuliza Mathew

“Ndiyo ni ya kwangu ninaimiliki kihalali kwa ajili ya ulinzi binafsi.Nilishauriwa

kuwa na silaha baada ya kutoweka kwa Kelvin” alijibu Regina

“Umewahi kuitumia silaha hiyo sehemu yoyote?

“Hapana sijawahi kuitumia hata mara moja” alijibu Regina

“Bastola hiyo wanadai ndiyo iliyotumiwa kumuua Amani na wale watu wengine katika nyumba yako.Hawa watu wanaokutafuta ni mtandao mkubwa uliojipanga vyema kukuangamiza kwa gharama zozote.Wanajua

kabisa kwa sasa baada ya kuhusishwa katika mauaji yale hauna sehemu ya kukimbilia lazima utakamatwa.Mtandao huu umekita mizizi yake hadi ndani ya serikali ndiyo maana mambo yamekuwa hivi.” Alisema Mathew

“Unanishauri nifanye nini?.Nikajisalimishe polisi? Sikufanya mauaji na wala sihusiki.” Alisema Regina

“Kwa sasa hutakiwi kufanya chochote.Utafuata kile nitakachokuelekeza kufanya.Simama nasi

tutakuondoa katika jambo hili.Kwa sasa endelea kujiandaa kwa ajili ya safari ya Dar es salaam”

“Jamani naombeni mnisaidie niwasiliane na mume wangu nimueleze ukweli anaweza akanisaidia kunitoa katika janga hili zito” alisema Regina

“Nilikueleza tangu jana kuwa kwa sasa hautawasiliana na mtu yeyote yule na hasa mume wako.Hawa wanaokutafuta lazima watakuwa macho kuwafuatilia

watu wako wa karibu wakiamini lazima utawasiliana nao.Ukithubutu kuwasiliana na yeyote wa karibu yako utakuwa umemuweka katika hatari kubwa" alisema Mathew na kutoka mle ndani akamfuata Ruby.

"Mathew hapa nilipo mwili wote unatetemeka.Sikutegemea kama jambo hili litakuwa kubwa namna hii" alisema Ruby

"Ruby tafadhali ondoa hofu.Tumekwisha ingia katika

vita lazima tupambane.Lazima tuhakikishe tunamuokoa Regina dhidi ya wale wanaotaka kumuua.Lazima tuhakikishe ile mipango yote miovu aliyoisema Regina ambayo inafanywa na chama chake tunaifahamu na kuhakikisha haifanikiwi.Nina kila sababu ya kuamini kile alichokisema Regina kuwa kipo.Papo hapo mwenzetu Gosu Gosu hatufahamu mahali alipo hivyo tuna jukumu la kuhakikisha tunamtafuta na kumtoa katika mikono ya hawa watu

tusiowafahamu.Nakuomba uwe na moyo wa kijasiri,tunakwenda kukutana na mambo mazito hivyo lazima tujiandae” alisema Mathew

“Ni kweli tutaondoka na Jombaa? Aliuliza Regina

“Ndiyo tunaondoka naye.Tukimuacha hapa lazima atakamtwa”

“Mathew huyu mtu ni jambazi sugu.Picha yake imesambaa kila mahali hivi sasa.Akionekana nasi anaweza akatuweka katika matatizo makubwa.Sidhani kama ni

jambo jema kuondoka naye.Atakuwa ni mzigo mzito kwetu” alisema Ruby

“Ruby usiwe na hofu yoyote.Huyu mtu anaweza akawa na msaada mkubwa kwetu.” Alisema Mathew

“Tutamtumiaje mtu kama huyu? Hata tukimchukua hawezi kutusaidia chochote.Anatafutwa na tutalazimika kumficha ndani.Nakuhakikishia Mathew kama tukiondoka na huyu mtu tutakuwa tumebeba nyoka mabegani ambaye atageuka na

kutugonga wenyewe.Tunatembea na mhalifu” alisema Ruby

“Ruby ondoa shaka kuhusu Jombaa.Tunaondoka naye” alisema Mathew.Alipiga simu kwa Peterson kuhusu usafiri akajulishwa kuwa tayari helkopta imekwisha ondoka Dar es salaam kueleka Arusha.Alimpigia simu vile vile rafiki yake mwingine ambaye ni meneja wa hoteli moja kubwa iliyoko nje ya jiji la Dar es salaam akamuomba helkopta watakayopanda ikatue katika hoteli

yake.Aliwasiliana pia na dereva wake akamtaka kupeleka gari sehemu Fulani kandoni mwa bahari.Alimpigia pia simu mtunza fedha wake akamtaka ampatie derva wake kiasi cha fedha kwa ajili ya matumizi yake.Alipomaliza kuwasiliana na watu muhimu aliowahitaji alizima simu yake.

***************

Safari ya usiku kucha ilizifikisha zile gari mbili katika nyumba moja iliyozungushiwa uzio wa rangi ya zambarau eneo la Matimu kwa Mzava jijini Dar es salaam.Kulikuwa na watu kadhaa mle ndani wakiwa wamevalia suti nzuri huku kila mmoja akiwa amejielekeza katika majukumu yake.Lango la gereji kubwa ambayo ilikuwa na uwezo wa kuhifadhi magari manne lilifunguliwa na magari yale mawili yakaingia ndani.Mlango mdogo

uliokuwemo ndani ya ile gereji ulifunguliwa wakaingia watu watatu wote wakiwa wamevali suti nadhifu.Mlango wa moja ya gari ulifunguliwa akashuka jamaa mmoja ambaye alisalimiana na wale jamaa wenye suti.Jamaa wengine waliokuwa katika magari walishuka.Baada ya mazugumzo mafupi ya dakika tano mlango wa nyuma wa moja ya gari ulifunguliwa jamaa aliyekuwa amefungwa mwili kwa kamba huku kichwani akiwa amevishwa

mfuko alishushwa akabebwa na kuingizwa ndani.

Chumba maalum kiliandaliwa ambamo yule jamaa aliingizwa.Ndani ya kile chumba kulikuwa na kitanda mithili ya kitanda cha kufanyia upasuaji ambacho kilikuwa na mikanda.Yule jamaa alilazwa juu ya kile kitanda kamba alizokuwa amefungwa mwilini zilikatwa.Mikanda migumu ya kitanda kile ilitumika kumfunga tena yule jamaa kiasi cha kutokufurukuta.Aliachwa ndani ya chumba kile akiwa

bado amefunikwa mfuko kichwani.

Baada ya dakika chache waliingia watu wengine wawili.Mmoja alikuwa amevaa suti ya kijivu alikuwa na sanduku lenye rangi nyeusi.Alilliweka mezani,akalifungua akatoa baadhi ya vifaa akaviweka mezani.Mfuko aliofunikwa yule jamaa ulitolewa.Alionekana kuchoka sana.Yule jamaa mwenye suti ya kijivu ambaye alionekana kama daktari alianza kumpima kwa kutumia vifaa vile

alivyokuja navyo.Aliandika katika kijitabu kila alipomaliza kumpima yule jamaa.Baada ya kukamilisha vipimo alivyovihitaji alichukua sampuli ya damu akarudisha vifaa vyake katika mkoba.Jamaa aliyekuwa amefungwa katika kitanda alivishwa tena ule mfuko mweusi.Daktari na yule aliyeongozana naye wakatoka ndani ya kile chumba.

Waliingia katika chumba kikubwa ambamo watu wawili walikuwa wamekaa katika sofa nzuri huku mmoja wao akiwa

na sigara mdomoni.Yule daktari alifunua kitabu chake alichoandika mambo kadhaa kuhusu vipimo alivyompima yule mtu mle chumbani.Baada ya kuwapa ripoti ile yule daktari alitoka na sanduku lake akaingia garini na kuondoka.

Baada ya daktari kuondoka jamaa wale wawili waliokuwa ndani ya kile chumba kikubwa waliendelea kujadiliana mambo kadhaa.Wakati wakiendelea kujadiliana ziliingia gari mbili.Kutoka katoka zile gari

vilishushwa vifaa mbali mbali ambavyo vilipelekwa katika chumba alimokuwa amefungwa yule mtu.Vifaa vile vilifungwa haraka haraka ikiwamo runinga kubwa ukutani na baada ya kukamilisha ufungaji wa vifaa vile walitoka nje.

Zilipita dakika ishirini daktari akarejea.Mkononi alikuwa na karatasi ndogo ambayo aliwapa wale jamaa wawili ambao bado walikuwa wanaendelea na majadiliano katika ile sebule kubwa.Baada ya kujadiliana wote waliinuka

wakaelekea katika chumba alimo yule jamaa aliyetolewa Arusha.Kwa mara nyingine tena daktari alimpima mapigo ya moyo halafu akawageukia wale jamaa akawapa ishara kwa kichwa kuwa mambo ni mazuri.

Mfuko aliovishwa yule jamaa ulitolewa kichwani

“Ndugu pole kwa safari ndefu.” Alisema mmoja wa wale jamaa mwenye suti.Mtu aliyefungwa kitandani alitoa ishara kuwa ana kiu anahitaji maji.

“Usiwe na wasi wasi sisi si makatili utapata kila unachokihitaji” alisema yule jamaa na kutoa maelekezo.Baada ya dakika mbili mlango ulifunguliwa wakaingia watu watatu mmoja akiwa amebeba sinia lililokuwa na chakula.Alifunguliwa mikono akainuka akakaa akaanza kula.Alikula huku akiwa amesimamiwa na watu watano.Alipomaliza kula alilitupa chini sinia lililokuwa na chakula.Wale jamaa walimtazama kwa hasira.

“Hiyo ndiyo ahsante yako? Aliiuliza yule jamaa mwenye suti akionekana kughadhabishwa na kitendo kile.

“Stupid ! alisema yule jamaa ambaye alionekana kupata nguvu baada ya kumaliza kula chakula

“Ahsante kwa kutuonesha wewe ni mtu wa aina gani.”

“Washenzi wakubwa ninyi ! alifoka tena yule jamaa kitandani.Wale jamaa walioleta chakula walielekezwa kumfunga tena yule jamaa

mikanda.Jamaa mmoja alimsogelea huku wenzake wakiwa wamezitoa bastola zao wakimuelekezea yule jamaa.Aliwatazama kwa dharau.

“Ndugu tafadhali usithubutu kuleta ubishi wowote.Tutakuharibu” alisema yule jamaa mwenye suti.Yule jamaa kitandani hakuleta ubishi alilala kitandani akafungwa tena mikanda halafu wale jamaa wakatoka.

***************

Geti la kuingilia Sangara Lodge lilikuwa wazi.Gari la akina Mathew lilipita getini na kuelekea katika maegesho ya magari.Ndani ya gari alikuwemo Mathew,Ruby na Regina.Pamoja nao alikuwemo pia Jombaa.Gari lilisimama, Jombaa akatumia simu ya Ruby akawasiliana na rafiki yake ambaye ni mmiliki wa hotel ile ambaye alitoka ofisini akawafuata maegesho.Jombaa alishusha kioo cha gari alipomuona huyo rafiki yake akamuita.

“Jombaa nini kinaendelea? Aliuliza yule rafiki yake akionekana kuwa na wasi wasi mwingi baada ya kumuona Jombaa amevaa mavazi ya kike.

“Pascal tutazungumza simuni baadae lakini mambo yangu yameharibika nadhani umeshasikia” alisema Jombaa

“Ndiyo nimesikia nikashtuka sana.”

“Kwa sasa ninaondoka kwa muda Arusha ili mambo yatulie halafu nitarudi.Hawa ni wenzangu niko nao na ndio

wanaonisaidia niweze kuondoka hapa Arusha.” Alisema Jombaa.Pascal alitazama pande zote kuona kama kuna watu eneo lile.

“Sitaki watu wakuone hapa.Naomba gari lisogezwe karibu kabisa na helkopta mimi nitalirudisha” alisema Pascal.Jombaa alimuongoza Mathew kueleka mahali ambako helkopta ilikuwa imetua.Kama alivyoelekeza Pascal gari lilisimamishwa karibu kabisa na helkpta lengo likiwa kumkinga Jombaa asionekane.Pascal alifika

mahali pale kwa haraka.Mathew alimpa maelekezo ya kulirejesha lile gari katika ile kampuni ya kukodisha magari halafu wakashuka garini.Jombaa ambaye alikuwa na jeraha mguuni alisaidia kushuka akaingizwa ndani ya helkopta .Mathew ndiye aliyekuwa wa mwisho kuingia.Pascal aliliondoa gari alilotumia akina Mathew na helkopta ikawashwa.Baada ya muda ilipaa na kuondoka.

***************

Mlango wa chumba ulifunguliwa kwa mara nyingine tena na safari hii aliingia mwanamama ambaye alimfanya yule jamaa aliyekuwa amefungwa katika kiti apandwe na hasira baada ya kumuona.

“Relax Gosu Gosu” alisema yule mwanamama kisha akavuta kiti akaketi.Gosu Gosu aliyekuwa amefungwa katika kile kitanda alimtazama kwa jicho baya.

“Endelea kunifunga hivi hivi lakini nikikuweka katika mikono yangu nitakutafuna nyama.Mimi ni mnyama zaidi ya wanyama unaowafahamu .Mimi si wa kufanyiwa hivi hata kidogo” alisema Gosu Gosu

“Gosu Gosu mimi na wewe bado tuna safari ndefu na hatutaachana hivi karibuni hivyo lazima ukubali ukaribu kati yetu.Mimi ndiye hatima ya maisha yako.Nikiamua kukupoteza ninakupoteza muda wowote niutakao.”

Alisema yule mama kwa kujiamini

“Ulinituma kazi nikaifanya.Hiki kinachoendelea hayakuwa makubaliano yetu.Huu moto uliouwasha utashindwa kuuzima.Umeniudhi sana Bernadetha.Njia pekee ya kuniepuka mimi ni kuzamisha risasi katika kichwa changu lakini ukiniacha hai ninakuhakikishia nitakutafuna nyama” alisema Gosu Gosu kwa ukali

“Siwezi kukuua Gosu Gosu kwa sababu bado ninakuhitaji sana na kazi yako haijakwisha.Tuache kutishana.Pole kwa safari ndefu.”alisema Bernadetha akionekana hana wasiwasi wowote.Alimtazama Gosu Gosu halafu akasema.

“Sasa tuzungume.Nilikutuma kazi Arusha,kwa nini uliniharibia kazi? Aliuliza Bernadetha

“Nilifanya kazi yako kama ulivyotaka” alijibu Gosu Gosu

“Hapana.Uliharibu kazi niliyokutuma.” Alisema Bernadetha akainua kichwa alitazama katika moja ya pembe za kile chumba ambako kulifungwa kamera.Alitoa ishara Fulani na hazikupita dakika mbili mlango ulifunguliwa akaingia mtu mmoja.

“Muoneshe kile alichokifanya” alisema Bernadetha.Yule jamaa aliwasha runinga iliyofungwa ukutani na video ikaanza kucheza.Walionekana watu watatu katika meza moja

wakiwa wamekaa wakizungumza.Mwangaza ulikuwa hafifu eneo lile lakini kamera iliweza kuwachukua wakaonekana vizuri.Video ile ilimalizika halafu ikasikika sauti ya Jombaa akisema

*“Nitahesabu hadi tatu kisha utamaliza mchezo.Tunatakiwa kuondoka hapa haraka sana”*

Jombaa alianza kuhesabu na kabla hajamalizia kutamka mbili ulisikika mlio wa risasi kutokea katika bunduki yenye kiwambo cha kuzuia sauti.

“Hapo ndipo tatizo lilipoanzia” alisema Bernadetha huku akimtazama Gosu Gosu

“Ulitakiwa usubiri hadi tatu lakini kabla Jombaa hajamaliza kutamka mbili ukaachia risasi” alisema Bernadetha

“Jombaa alikuelekeza mtu wa kwanza kumuua awe ni yule mwanamke lakini wewe ulikwenda kinyume ukamuua mtu mtu mwingine ambaye hata kama angebaki hai asingekuwa na madhara

yoyote.Tunayo rekodi ya tukio zima.Baada ya kuipitia rekodi hiyo kuna mambo tumeyabaini.Kubwa ambalo tumelibaini kwanza hukutaka kumuua yule mwanamke na nitakwambia kwa nini hukutaka mwanamke yule afe.Ulimpiga yule jamaa risasi ya kwanza shingoni risasi ambayo ulipaswa kumpiga kichwani.Kama  haitoshi ulimuongeza risasi ya pili ambayo ulipaswa kumpiga yule mwanamke.Risasi ya tatu ambayo ulipaswa kumpiga yule jamaa mwingine

aliyejitokeza katika ile meza uliipoteza kwa kupiga chupa.Wale watu wengine wawili wakashtuka wakafanikiwa kukimbia.Uliharibu kazi makusudi.Nitataka unipe jibu kwa nini uliharibu kazi? Kwa nini hukutaka kumuua yule mwanamke?” alisema Bernadetha huku akiendelea kumkazia macho Gosu Gosu

“Wakati tukiendelea kufanya uchunguzi kuhusiana na kile ulichokifanya, kuna kitu tulikibaini.Mtu yule wa tatu ambaye alikuwa katika ile

meza hakufika pale kwa bahati mbaya" alisema Regina na katika runinga ikatokea picha ya Mathew Mulumbi.Gosu Gosu alihisi mwili wote unaisha nguvu.

"Unamfahamu huyu mtu? Aliuliza Bernadetha.

Gosu Gosu aliitazama picha ile ya Mathew akajitahidi asioneshe mshangao wowote

"Hapana simfahamu huyu mtu."

"Una uhakika humjui huyu mtu? Aliuliza Bernadetha

“Nimekwambia simfahamu.Unataka nitumie lugha ipi unielewe? Aliuliza Gosu Gosu kwa ukali.

“Huna haja ya kuwa mkali.Tutakwenda taratibu tutaelewana” alisema Bernadetha.Katika runinga ilitokea tena picha nyingine Gosu Gosu akiwa na Mathew.

“Unasemaje kuhusu picha hii? Bado humfahamu huyu mtu? Aliuliza Bernadetha.Gosu Gosu aliitazama tena ile picha safari

hii kwa umakini mkubwa halafu akasema

“Simfahamu huyu mtu.”

“Wewe una kichaa? Alifoka Bernadetha

“Wewe ndiye mwenye kichaa kunilazimisha kumkubali mtu nisiyemfahamu” alisema Gosu Gosu

“Wewe ni jeuri sana.Huyu pichani ni nani?

“Sura inafanana nami lakini si mimi” alijibu Gosu Gosu

“Si wewe? Aliuliza Bernadetha kwa ukali

“Si mimi.Tafadhali sitaki uendelee kunilazimisha nikubali kitu nisichokifahamu.Huyu mtu simfahamu na wala hii si picha yangu! Alisema Gosu Gosu kwa ukali.Bernadetha alimtazama Gosu Gosu kwa hasira.

“Nakuuliza kwa mara nyingine tena huyu katika picha si wewe?

“Hapana si mimi.Simfahamu huyu mtu”

alijibu Gosu Gosu bila kupepesa macho.

"Huyu anaitwa Mathew Mulumbi.Ni mwenyekiti wa Mulumbi group of companies.Hata kampuni ya kusindika maziwa ambayo wewe ni mkurugenzi, mmiliki wake ni Mathew Mulumbi. Aliwahi kufanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania.Ni mmoja wa wapelelezi nguli kabisa kuwahi kutokea hapa nchini.Bado unakana kuwa humfahamu huyu mtu? Aliuliza Regina

“Je ne le connais pas” alijibu Gosu Gosu akitumia lugha ya kifaransa

“Labda nitumie lugha ya kigeni ndipo utanielewa ninapokwambia kwamba simfahamu huyo mtu unayemsema.” Aliongeza Gosu Gosu.

“Huyu mtu maskani yake ni Dar es salaam lakini ghafla tu amefika Arusha na kumtafuta yule mwanamke ambaye ulitakiwa kumuua.Kama haitoshi usiku ambao Regina alitakiwa

kuawa,Mathew Mulumbi anajitokeza tena na kukaa naye meza moja.Hii ni sababu iliyokufanya ukaharibu kazi.Hukutaka kumuua Mathew wala Regina.Hii ni picha ya wazi kwamba ule ulikuwa ni mpango uliopangwa." Alinyamaza Regina akiendelea kumtazama Gosu Gosu.

"Kuna jambo lingine.Katika chumba cha mtu wa kwanza uliyemuua kuna vitu vilikosekana.Simu ya yule jamaa haikupatikana vile vile kadi ya kuhifadhi picha

katika kamera nayo pia ilikosekana.Tukiunganisha kuhusu kupotea kwa vifaa hivyo na kile kilichotokea katika tukio la pili,tunaamini kabisa vitu vile ulivichukua wewe kwa madhumuni unayoyafahamu mwenyewe.Nafahamu nikikuuliza kama hayo niliyoyasema ni ya kweli utakana kama ulivyoikana picha yako wewe mwenyewe.Ninataka kukuthibitishia kuwa sisi si watu wa kukurupuka.Tunakufahamu

zaidi ya unavyojifahamu Gosu Gosu.Nimekuleta hapa kwa ajili ya kufahamu ukweli.Kwanza nataka kujua vitu vile ulivyochukua kutoka kwa yule mtu uliyemuua viko wapi? Aliuliza Regina.

“Tuoneshe vilipo ili tuyamalize mambo haya.Hatuna haja ya kukufanyia ukatili.Tunachohitaji sisi ni kuvipata vitu vile ambavyo ni muhimu sana kwetu.Viko wapi? Aliuliza Bernadetha

Gosu Gosu alitoa kicheko kidogo halafu akasema

"Kwanza kabisa nataka kufahamu kwa nini mnanitumia mimi kufanya kazi zenu? Wapo watu wengi tu ambao mngeweza kuwakodisha wakawafanyia kazi yenu kwa nini mkawaacha wote mkanichagua mimi? Aliuliza Gosu Gosu

"Gosu Gosu sihitaji utani.Ninaomba unijibu swali nililokuuliza" alifoka Bernadetha

“Ambola anafahamu hiki unachonifanyia? Aliuliza Gosu Gosu

“Shut up ! alifoka Bernadetha huku akiinuka

“Mara ya mwisho kabisa nieleze ni wapi vilipo vile vitu ulivyovichukua ndani ya kile chumba? Aliuliza Bernadetha.

“Safari hii nitazungumza Kireno kwa sababu nilipozungumza Kifaransa naona hukunielewa” alisema Gosu Gosu huku akimtazama Bernadetha kwa dharau

Bernadetha akiwa amefura hasira alitoka ndani ya kile chumba na baada ya dakika chache akarejea akiwa ameongozana na jamaa wawili waliojaza miili yao.

“Kazi kwenu vijana.Nataka azungumze kila kitu” alisema Bernadetha.

Ile mitambo yote iliyofungwa  awali ilikuwa maalum kwa ajili ya kutesea.Mrija wenye sindano uliunganishwa katika mshipa wa damu na mashine zikawashwa.Dawa maalum

kwa ajili ya kuleta maumivu makali mwilini ilichomwa katika ule mrija uliounganishwa katika mshipa wa damu na taratibu dawa ile ilianza kuingia katika mwili wa Gosu Gosu.Wale jamaa wawili walikuwa makini sana kufuatilia katika runinga mbili ndogo.Dawa ile ilianza kuingia katika mwili wa Gosu Gosu akaanza kuhisi maumivu makali.Maumivu yalizidi na Gosu Gosu alianza kugugumia .Alihisi kama mwili wake unawaka moto.

“Tafadhali Gosu Gosu tueleze vilipo vile vitu ulivyochukua ndani ya kile chumba” alisema Bernadetha.Bado Gosu Gosu hakuwa tayari kusema ukweli.Kiwango cha dawa kilichopimwa kiliingia chote ndani ya mwili wa Gosu Gosu.Macho aliyafumba kutokana na maumivu makali aliyoyapata.Alihisi yuko ndani ya tanuru la moto.

“Uko tayari kuzungumza ukweli Gosu Gosu? Aliuliza Bernadetha.Bado Gosu Gosu aliendelea kugugumia kwa

maumivu makali.Hakuthubutu kufumbua mdomo wake kusema chochote.

“Kwa nini unateseka Gosu Gosu.Utapungukiwa nini kusema ukweli kwamba ulichukua vile vitu na kuonesha mahali vilipo? Tuoneshe mahali vilipo ili tuiondoe dawa mwilini mwako ama sivyo tutaongeza kiwango.” Alisema Regina

Pamoja na maneo yale ya ushawishi kutoka kwa Regina bado Gosu Gosu hakuwa tayari kusema chochote.

“Nimepitia mateso makali sana huko nilikotoka lakini sijawahi pata maumivu kama haya.Ni kama vile nimerushwa katika shimo la moto.Pamoja na maumivu haya kamwe sintakubali kumuuza Mathew Mulumbi.Niko tayari kufa kuliko kuwasaidia hawa watu wakampata Mathew” aliwaza Gosu Gosu

“Gosu Gosu nakuomba kwa mara ya mwisho unieleze ukweli au nioneze dawa” alisema Bernadetha.Gosu Gosu hakujibu kitu.Bernadetha aliwapa

maelekezo wale jamaa waongeze dawa.

Dawa ilipoanza kuingia mwilini Gosu Gosu alihisi kama vile ngozi yake inaachana na nyama.Yalikuwa ni maumivu makali mno.Pamoja na maumivu yale makali lakini hakufumbua mdomo wake kusema chochote.Bernadetha aliishuhudia dawa ikiendelea kumalizika katika bomba la sindano ikiingia katika mwili wa Gosu Gosu.Alimtazama kwa mshangao mkubwa.

“Haya ni maajabu makubwa sana.Haijawahi kutokea mtu akamaliza awamu ya kwanza ya dawa hii bila kuamua kufunguka ukweli.Huyu ni kiumbe wa aina gani ambaye amemaliza awamu mbili bila kufungua mdomo wake? Huyu ni zaidi ya mwanajeshi” aliwaza Bernadetha.Aliendelea kumshuhudia Gosu Gosu akijinyonga nyonga kwa maumivu makali.

“Gosu Gosu hapa ndiyo kwanza tumeanza.Tutaongeza kiwango cha dawa na utajihisi

uko jehanamu.Tunachohitaji ni kitu kidogo mno.Tujibu maswali yetu machache ili tusiendelee kukutesa.” Alisema Bernadetha kwa sauti ya kubembeleza.Gosu Gosu hakuonesha dalili zozote za kufungua mdomo wake kusema chochote.Bernadetha aliwataka wale jamaa watoke nje ya kile chumba.

“Huyu mtu ni mgumu mno.Ni mwanajeshi.Anayafahamu mateso na anaweza kuhimili kila aina ya mateso.Ninyi wenyewe ni mashahidi

hajawahi mtu kumaliza hata awamu ya kwanza ya dawa lakini huyu amemaliza awamu mbili.”

“Si mtu wa kawaida huyu” aliongeza mmoja wao

“Ninataka tuingie katika awamu ya tatu vile vile tuongeze kiwango cha dawa” alisema Bernadetha.

“Madam haitawezekana.Tukiongeza awamu nyingine tutamuua.Tunatakiwa kusubiri kwa saa sita kabla ya kumchoma tena dawa

nyingine.” Alisema mmoja wa wale jamaa.

“Ninasema ongeza dawa nyingine.Huyu mtu lazima afunguke leo! Alifoka Bernadetha

“Madam hata daktari alielekeza hivyo kwamba tusizidishe kiwango cha dawa na wala isizidi awamu mbili.” Alisema yule jamaa

“Mimi ndiye ninayemlipa huyo daktari.Ninasema lazima kuingia awamu ya tatu hata ya nne kama itawezekana.Ninachohitaji ni

kumfungua huyu mtu.Ana mambo muhimu sana ambayo lazima tuyafahamu”alifoka Bernadetha.Jamaa mmoja aliingia ndani ya kile chumba akatoka na bomba la sindano pamoja na chupa mbili za dawa akampatia Bernadetha.

“Nini maana yake hii? Aliuliza Bernadetha

“Ninakupatia dawa umchome wewe mwenyewe na kwa kiwango unachokihitaji” alisema yule jamaa.Bernadetha alimtazama kwa jicho kali halafu akasema

“Sawa mpumzisheni kwa muda.Andaeni Plan B”alielekeza Bernadetha akaenda katika chumba cha mapumziko akachukua simu yake akaitafuta namba Fulani akapiga.

“Imeshindikana.Hatujapat a chochote bado.Yule mtu ni mgumu mno kufunguka.Kwa sasa tunaingia katika plan B.Nitakujulisha kile kitakachotokea” alisema Bernadetha na kukata simu.Alivuta pumzi ndefu akaegemeza kichwa sofani.

“Sikulikubali wazo la kumtumia huyu jamaa katika kazi hii na haya ndiyo matokeo yake.Ameharibukila kitu.Mathew Mulumbi kuingia katika suala hili ni hatari sana kwetu.Yule si  mtu mzuri hata kidogo.Nimfahamuvyo yule mtu akinusa harufu ya kitu Fulani ataifuatilia hadi mwisho.Nina uhakika kabisa kuwa lazima kuna kitu amekinusa kuhusu mpango ule wa kumuua Regina.Kuondoka Dar na kwenda Arusha kumtafuta Regina tena akitumia jina bandia si kwa

bahati mbaya.Kuna jambo.Kwa namna yoyote lazima naye apatikane kwa haraka.” Aliwaza Bernadetha.Alitolewa mawazoni na mmoja wa jamaa aliyeingia mle ndani akamjulisha kuwa kila kitu kwa ajili ya Plan B kiko tayari.Bernadetha aliinuka akaelekea katika chumba alimo Gosu Gosu

Bado alikuwa ameyafumba macho yake akiendelea kusikilizia maumivu makali.Bernadetha alimsogelea akamtikisa

kichwa.Gosu Gosu alifumbua macho.Sehemu ya kitanda upande wa kichwani iliinuliwa.

“Tazama runinga tafadhali” alisema Bernadetha.Gosu Gosu pamoja na maumivu aliyokuwa nayo aligeuza shingo akatazama runingani kama alivyoelekeza Bernadetha.Ghafla Gosu Gosu alihisi maumivu yote aliyokuwa nayo yakitoweka baada ya kushudia kitu runingani.

“Hiki ni kitu cha kweli ninakiona au ninaota? Alijiuliza

“Gosu Gosu muda wa kubembelezana umekwisha.Nafahamu unampenda sana Ambola.Ni wakati wako wa kudhihirisha namna unavyompenda.” Alisema Bernadetha

“Nini sababu ya kumfanya hivi mtoto wako mwenyewe? Aliuliza Gosu Gosu.

“Hatima ya Ambola iko mikononi mwako.Nikitoa amri muda wowote atauawa huku

ukishuhudia.Ninataka umpigie simu Mathew Mulumbi na kumuuliza mahali alipo" alisema Bernadetha halafu akampa jamaa mmoja maelekezo akatoka.Baada ya dakika chache akarejea akiwa na sanduku jeusi pamoja na simu ambayo alimpatia Bernadetha.Sanduku lile lilifunguliwa na ndani yake kulikuwa na kompyuta na vifaa vingine.Kila kitu kiliwekwa tayari.

"Gosu Gosu ninampigia simu Mathew kwa kutumia simu yako halafu nitakupa

uzungumze naye.Uko tayari kwa hilo au Ambola auawe? Aliuliza Bernadetha.Gosu Gosu alimtazama kwa hasira

“Aaagghh ! alipiga ukelele huku akijaribu kujitikisa lakini mikanda imara ya kitanda kile ilimshika barabara hakuweza kufurukuta.

“Please stop this.Unawezaje kumfanyia hivi mwanao? Aliulza Gosu Gosu.Runingani Ambola alikuwa amepiga magoti akiwa ameshikiliwa na jamaa wawili waliovaa kofia zilizoficha sura

zao.Jamaa mwingine alikuwa pembeni akiwa na bastola.

Bernadetha hakumjibu kitu badala yake aliwasha simu ya Gosu Gosu halafu akafungua sehemu ya kuhifadhi namba za simu.Alilipata jina limeandikwa M.Mulumbi.Aliipigia namba ile.Alikunja uso baada ya namba ile kutokuwa hewani.

“Bastard ! alifoka

“Namba nyingine ya Mathew ni ipi? Aliuliza Bernadetha.Gosu Gosu

hakumjibu kitu.Bernadetha alijaribu zaidi ya mara tatu kuipiga namba ile bila mafanikio.

“Hapatikani.Nataka uniambie ni wapi tutampata Mathew? Hilo ni swali la mwisho nitakuuliza na kama ukishindwa kulijibu Ambola mwanamke unayempenda atauawa huku ukishuhudia” alisema Bernadetha.Gosu Gosu alifumba macho huku sura yake ikiwa imejikunja kwa hasira.

“Gosu Gosu una sekunde kumi tu za kufanya maamuzi.Chagua aidha Mathew Mulumbi au Ambola mwanamke umpendaye” alisema Bernadetha.

Gosu Gosu alifumbua macho akamtazama Bernadetha kwa macho yaliyojaa hasira halafu akasema.

“Go ahead.Kill her.Ambola hana maana yoyote kwangu” alisema Gosu Gosu.Bernadetha hakuamini masikio yake.Alimtazama

Gosu Gosu kwa hasira kali halafu kwa sauti kubwa akasema.

“Endeleeni na zoezi” alisema halafu akatoka ndani ya kile chumba akiwa amefura hasira.Alienda katika chumba cha mapumziko akatoa simu akaitafuta namba ya kamanda wa polisi mkoa wa Arusha.

“Kamanda habari ya saa hizi? Aliuliza Bernadetha baada ya simu yake kupokelewa

“Madam kuna mafanikio yoyote?aliuliza kamanda wa polisi mkoa wa Arusha

“Hakuna chochote tumekipata.Huyu jamaa ni mgumu mno kusema chochote.Simu ya Mathew Mulumbi haipatikani.Nina uhakika mkubwa bado yuko jijini Arusha.Tulituma watu katika makazi yake kufanya uchunguzi tukajiridhisha Mathew hayupo.”

“Tangu usiku wa jana njia zote za kuingia na kutoka arusha tumeweka vizuizi na

ukaguzi mkali unafanyika katika kila gari linaloingia na kutoka.Mpaka muda huu sijapata taarifa yoyote ya kupatikana kwa Mathew,Jombaa au Regina.”alisema kamanda wa polisi

“Kamanda ongeza ulinzi tafadhali.Mathew hatakiwi kutoka nje ya Arusha.Yule mtu ni hatari kubwa.Akinusa harufu ya kitu lazima atakifuatilia hadi chanzo chake.Tayari kuna kitu amekifahamu.Tunaendelea kumuhoji huyu mwenzake

hapa ili kujiridhisha kama hajamwambia chochote Mathew.Msako wa Jombaa umefikia wapi? Aliuliza Bernadetha

“Mpaka sasa hakuna anayejua mahali alipo.Kuna wenzake kadhaa ambao tumejaribu kuwadadisi lakini hakuna anayefahamu yuko wapi.Tunaendelea kumsaka ninaamini baada ya picha yake kusambaa kila mahali wananchi watatujulisha mara moja akionekana.Nina uhakika mkubwa yuko mahali amejificha hapa hapa Arusha”

alisema kamanda wa polisi wa mkoa wa Arusha

“Sawa kamanda endeleeni na msako na chochote mtakachokipata naomba unijulishe tafadhali” alisema Bernadetha na kukata simu.

**************

Hakuna mtu aliyeitilia maanani helkopta iliyotua katika kisiwa cha Ngwazu kilichopo katika bahari ya Hindi kilometa kadhaa kutoka jijini Dar es salaam.Kisiwa cha

Ngwazu ni mahali kwenye utulivu mkubwa ambako wageni wengi hupenda kwenda kupumzika katika ufukwe mzuri.Hoteli kubwa ya kitalii ilijengwa katika kisiwa hicho na kukifanya pawe ni sehemu yenye kuvutia sana.

Helkopta ilitua katika sehemu yake maalum.Baada ya injini kuzimwa jamaa mmoja mwenye asili ya kiarabu akiwa amevalia suti nadhifu aliisogelea ile helkopta.Mlango ulifunguliwa na wa kwanza kushuka alikuwa ni Mathew ambaye

alisalimiana na yule jamaa ambaye alimpa maelekezo Fulani halafu akaondoka kwa haraka kuelekea katika gati.Mathew aliwataka akina Ruby washuke.Regina alijitanda vazi lililomfunika mwili mzima isipokuwa macho.Jombaa naye alivaa vazi kama lile kiasi kwamba haikuwa rahisi kujulikana kama ni mwanaume.Bado Jombaa alikuwa katika maumivu lakini Mathew alimtegemeza akamsaidia kutembea.Walitembea taratibu kuelekea katika gati ambako

kulikuwa boti imeegeshwa. Waliingia katika boti ile,Mathew aliagana na yule kijana kisha safari ikaanza kuelekea jijini Dar es salaam katika ofisi za hoteli ile ambako angekutana na dereva wake.

**************

Hatimaye Mathew na watu wake waliwasili salama katika moja ya nyumba ya Mathew iliyopo eneo la bwawa Tina.Eneo hilo liliitwa bwawa Tina kutokana na uwepo wa bwawa kubwa la kuchimbwa

linalotumiwa kufuga samaki ambalo linamilikiwa na mzungu anaitwa Chritsina.Kwa kufahamu kuwa maisha yake yamezungukwa na hatari nyingi ,Mathew amekuwa na kawaida ya kujenga nyumba sehemu mbali mbali kwa ajili ya usalama wake pale anapokuwa katika matatizo.

Geti la nyumba lilifunguliwa na mtu ambaye alikuwa muangalizi wa ile nyumba ambaye alijengewa nyumba ya kuishi mita kama hamsini kutoka ilipo nyumba

kubwa ya ghorofa mbili.Tangu akiwa Arusha Mathew alimjulisha Zakaria muangalizi wa nyumba yake kuwa atafika pale.

Mathew alimshukuru dereva wake na kumtaka aende akapumzike ila gari aliliacha pale kwa ajili ya Mathew kulitumia.Baada ya dereva kuondoka,Mathew alizungumza na Zakaria akamjulisha kuwa atakuwepo pale katika nyumba yake kwa siku kadhaa hivyo akamuomba Zakaria kwenda nyumbani kwao kwa mapumziko ya wiki

mbili.Alimpatia kiasi cha pesa kutoka katika fedha alizoletewa na dereva wake.

“Jamani karibuni sana.Hii ni moja ya nyumba zangu za siri.Nina kawaida ya kuwa na nyumba za siri kwa sababu maisha yangu yamezungukwa na hatari nyingi hivyo kila ninapokuwa katika kitisho chochote hutafuta moja ya nyumba zangu nikaenda kujificha huko.” Mathew aliwaambia akina Ruby

“Tumefika Dar es salaam.Nini kinaendelea hapa?

Aliuliza Regina wakati Mathew akimuonesha chumba chake cha kulala.

“Tunaamini chimbuko la mipango yote ya kukuua ni hapa Dar es salaam ndiyo maana tumekuja huku.Tunaanza uchunguzi wetu kuwasaka na kuwafahamu wale wote wanaotaka kukuua vile vile kuifahamu mipango yao yote.Ninakutoa hofu,hapa uko sehemu salama sana.Tutakulinda kwa gharama zozote” alisema Mathew

“Mathew ninakushukuru sana kwa yote uliyonifanyia tangu Arusha.Bila wewe hivi sasa ningekuwa marehemu.Pamoja na hayo yote kuna kitu kimoja ambacho kinanipa hofu kubwa.Huyu jamaa aliyetaka kuniua kwa nini yuko hapa? Nina hofu sana kukaa na mtu huyu nyumba moja” alisema Mathew

“Usiwe na hofu Regina nimekwisha kuhakikishia usalama wako.Yule jamaa alikodishwa tu kufanya mauaji yale na kwa sasa hata yeye

anasakwa na jeshi la polisi ndiyo maana tuko naye hapa.”

“Unadhani itachukua muda gani uchunguzi wa kuwabaini wale wanaotaka kuniua kukamilika?Hofu yangu nyingine ni kwamba ninasakwa na jeshi la polisi je hawatabaini kama niko hapa?Aliuliza Regina

“Kwanza kabisa katika uchunguzi wetu sisi hatushirikiani na jeshi la polisi au chombo kingine chochote hadi pale inapolazimika kuwa hivyo.Tunachunguza kimya

kimya na baada ya kuufahamu ukweli na kuwakamata watuhumiwa ndipo huwakabidhi kwa jeshi la polisi pamoja na ushahidi wote tulioupata.Kuhusu ni muda gani utakaa hapa hilo siwezi kuwa na jibu kwa sababu hakuna muda maalum wa kufanya uchunguzi.Kwa sasa endelea kupumzika.Kila unachokihitaji tuambie utakipata.Kila tutakachokipata tutakuwa tunakujulisha” alisema Mathew na kutoka mle chumbani akaenda

kumuonesha pia Jombaa chumba atakachokitumia.

“Jombaa dhumuni la kukuleta hapa ni kukusaidia usikamatwe na polisi hivyo utaishi humu ndani hadi pale mambo yatakapotulia.Chochote unachokihitaji tuambie tutakupatia lakini usithubutu kutoka nje.Humu ndani kuna kila kitu unachokihitaji.Kama unahitaji kupunga hewa utaenda upande wa nyuma kuna bwawa la kuogelea utapumzika huko.” Alisema

Mathew na kutoka akamfuata Ruby

“Ruby sisi hatuna muda wa kupumzika.Tunaanza kazi mara moja.” Alisema Mathew wakiwa katika chumba maalum kilichotengwa kwa ofisi.

“Tunaanzia wapi Mathew? Aliuliza Ruby

“Kabla ya kujua wapi tuelekee hebu kwanza tulichambue tukio zima lilivyo ili tujue wapi tuanzie.” Alisema Mathew huku Ruby akiweka kompyuta yake sawa.Mathew

alilifungua faili lenye picha mbali mbali ambazo Ruby alikuwa amezichapisha akaichukua picha moja akaenda kuibandika katika ubao mkubwa.

“Mambo yalianzia kwa huyu Anganile bandia.Huyu ametumia jina bandia na tunaamini alikuwa anamchunguza Regina.” Alisema Mathew na kuichukua picha ya pili akaibandika chini ya picha ya Anganile bandia

“Kutoka kwa Anganile bandia anakuja huyu ambaye

ni Gavana wa benki kuu Jackson Mzumile.Huyu aliwasiliana na Anganile bandia na tunahisi labda ni yeye aliyemtuma Arusha kumchunguza Regina” alisema Mathew halafu akaenda tena kwenye faili akaichukua picha nyingine akaibandika pembeni ya picha ya gavana.

“Regina anahisi sababu ya yeye kuchunguzwa na gavana ni kutokana na kupotea kiajabu kwa huyu mwanae Kelvin.” Alisema Mathew akasimama akazitazama picha zile kwa sekunde kadhaa.

“Katika upande huu,Anganile bandia na Kelvin hawapo hivyo basi mtu ambaye anaweza akatupa majibu ni Gavana.” Alisema Mathew akaenda kuichukua picha nyingine akaibandika ubaoni.

“Huu ni upande wa pili.Tunaanza na Regina Zanga.Huyu anatakiwa kuuawa.” Alisema Mathew akachukua tena picha nyingine akaibandika ubaoni.

“Papi Gosu Gosu.Huyu ndiye aliyetakiwa kumuua

Regina.Hatuna bado picha ya mama yake Ambola” alisema Mathew na kuchukua karatasi tupu akaibandika ubaoni akaandika mama Ambola.Aliichukua karatasi nyingine akaandika Ukombozi wa Afrika akaibandika ubaoni.

“Regina anahisi wanaotaka kumuua ni wenzake ndani ya chama baada ya kuzifahamu siri za chama.” Alisema Mathew akazitazama picha zile halafu akasema

“Mtu wa kwanza kabisa ambaye tunatakiwa kumfanyia

uchunguzi ni mama yake Ambola.Huyu ndiye aliyemtengenezea mtego Gosu Gosu akamlazimisha kwenda Arusha kumuua Regina.Huyu mama hatuna mawasiliano yake na wala hatumfahamu kiundani.Mtu pekee ambaye anaweza akatusaidia kumpata ni Ambola.Tutamfuata katika sehemu yake ya biashara.Kazi ya pili ya kufanya ni kutafuta nafasi ya kuonana na Gavana kuzungumza naye kuhusiana na yule Anganile bandia kama ni yeye aliyemtuma kumchunguza Regina ”

Alisema Mathew na maandalizi ya kwenda kuonana na Ambola yakaanza.

**************

Mathew na Ambola walifika katika mgahawa wa Ambola ambao ni maarufu kwa kuuza Pizza jijini Dar es salaam.Geti la kuingilia mahali hapo lilikuwa limefungwa na kuliwekwa kibao chenye maandishi makubwa CLOSED.Hakukuwa na shughuli yoyote iliyoendelea katika mgahawa huo.Mathew

alishuka garini akamfuata mlinzi aliyekuwa amevaa sare za ulinzi suruali nyeusi na shati jeupe.Alimsalimu na kumuuliza.

“Mkuu, hawa watu wako leo? Hawafungui? Aliuliza Mathew

“Ni siku ya pili leo hakuna mtu mahali hapa.Nimeambiwa wamefunga kwa muda kuna mambo wanayafanya.Sifahamu zaidi ya hapo” alijibu yule mlinzi.

“Viongozi wao wamefika hapa baada ya mgahawa kufungwa ? Aliuliza Mathew

“Hakuna mtu yeyote aliyefika hapa tangu mgahawa ulipofungwa.” Alijibu yule mlinzi.

“Nina shida na meneja.Unaweza kufahamu mahali anakoishi? Aliuliza Mathew

“Hapana sifahamu.Mimi ni mlinzi tu mambo mengine siyajui”

“Ahsante sana ndugu yangu” alijibu Mathew na kurejea garini akamueleza Ruby kile kilichotokea

“Kwa nini wamefunga mgahawa?Ruby aliuliza

“Hakuna mwenye jibu la uhakika ila swali lingine ambalo tunatakiwa kujiuliza kwa nini wafunge sasa?Kuna tatizo gani? aliuliza Mathew huku akiwasha gari.Wakati wakisubiri kuingia barabara kuu,Mathew akamtaka Ruby kuitafuta tovuti ya mgahawa ule maarufu jijini Dar es

salaam.Ruby aliikunjua kompyuta yake akaanza kazi.Mathew alifanikiwa kuliingiza gari barabara kuu na tayari Ruby alikuwa ameipata tovuti ya mgahawa ule.

“Hapa kuna namba ya mkurugenzi wa hoteli na nyingine ya huduma” alisema Ruby

“Andika namba ya simu ya meneja mpigie kwa kutumia simu yako.” Alisema Mathew na bila kupoteza muda Ruby aliiandika namba ya simu ya meneja

akampigia.Alishtushwa na jibu alilopewa baada ya kupiga simu

*“Samahani.Namba ya simu unayopiga haipo.Tafadhali angalia namba kwa usahihi kisha jaribu tena”*

Ruby aliitazama namba ile kama imekamilika akajaribu kuipiga lakini jibu lilikuwa lile lile kwamba namba ile haipo.

“Haya ni maajabu.Ninaambiwa namba hii haipo” alisema Ruby

“Inawezekanaje wakaiweka namba katika tovuti namba ambayo haitumiki? Aliuliza Mathew.

“Nina rafiki yangu anafanya kazi katika mtandao huu wa simu.Ngoja nimpigie anisaidie kujua kama namba hii ina tatizo lolote” alisema Ruby akampigia rafiki yake ambaye anafanya kazi katika kampuni ya simu akamtaka amsaidie kujua kama ile namba ina tatizo lolote.Baada ya dakika tatu alipigiwa simu na kupewa jibu ambalo lilizidi kuwachanganya.Namba ile

haikuwepo.Ndivyo alivyosema rafiki yake Ruby.

“Clara una hakika namba hii haikuwahi kusajiliwa kabisa katika mtandao wenu? Ruby aliuliza

“Siwezi kukudanganya Ruby.Namba hii haipo kabisa katika rekodi zetu.Yawezekana aliyekupa namba hii amekosea” alijibu Clara.Ruby hakuwa na swali lingine alimshukuru Clara halafu akakata simu.

“Mathew mbona ninazidi kushangazwa na haya

mambo.Clara anadai namba hii haipo na hawajawahi kuisajili.Inawezekanaje? aliuliza Ruby

“Hilo ni swali la msingi sana.Namba hii iliwekwa katika tovuti na ndiyo iliyokuwa ikitumika kwa mawasiliano na meneja.Hatuwezi kujua yawezekana labda haikutumika muda mrefu na ikafutwa.Kwa sasa tunatakiwa kujua mahali anakoishi ili tumfuate” alisema Mathew

“Gosu Gosu aliwahi kukuelekeza mahali anakoishi mpenzi wake? Aliuliza Ruby

‘Hapana.Hakunieleza.Ila kuna dada mmoja ambaye nilikutana naye katika sherehe ile ya Ambola anaitwa Salma.Nilikaa naye meza moja na katika mazungumzo alinielekeza mahali anakofanyia kazi akanipa na namba yake ya simu.Alidai Ambola ni rafiki yake sana” alisema Mathew

“Wewe nawe yaani kukutana tu tayari

umeshachukua hadi namba ya simu ! alisema Ruby

"Ni kwa ajili ya mawasiliano tu.Ninapenda kutengeneza marafiki wapya kila siku kwani huwezi kujua nani anaweza akawa na msaada kwako" alisema Mathew huku gari ikiwa katika mwendo mdogo.Aliuzungusha mkono katika mfuko wake wa nyuma wa suruali akatoa pochi ndogo akampatia Ruby ili aitafute kadi ya biashara aliyopewa na Salma.Ruby aliipata halafu akaiandika

namba ya simu ya Salma katika simu yake akapiga.

“Hallow” ilisema sauti ya upande wa pili.Mathew akaichukua simu.

“Hallow Salma habari yako? Mimi ni Mathew tulikutana katika sherehe pale Patra hotel.Unanikumbuka? aliuliza Mathew

“Ouh Mathew ! Ninakukumbuka sana.Ahsante kwa kunikumbuka” alisema Salma

“Salma ninaweza kukuona kwa dakika chache kama hutajali? Mathew aliuliza

“Hapana sintajali lakini kwa sasa nipo kazini.Saa ngapi unataka tuonane? Aliuliza Salma

“Niko njiani ninakuja kazini kwako.Kama hutajali ninataka kukuona kwa dakika tatu tu”

“Haya karibu.Ukifika nijulishe nikufuate” alisema Salma na kukata simu.

“Anafanya kazi gani huyu Salma?

“Anafanya kazi katika duka la kubadili fedha” alijibu Mathew na safari ikaendelea.

Iliwachukua dakika kumi na sita kufika katika duka la kubadili fedha za kigeni anakofanya kazi Salma.Wakiwa maegesho,Mathew alimpigia tena simu Salma akamjulisha kuwa tayari amefika.Salma alitoka na mara Mathew alipomuona akashuka garini wakakutana.

“Samahani sana Salma kwa kukusumbua” alisema Mathew

“Usijali Mathew.Habari za tangu siku ile tulipokutana? Aliuliza Salma

“Salma sitaki kuchukua muda wako mwingi nina jambo dogo nataka unisaidie”

“Jambo gani? aliuliza Salma

“Siku ile uliniambia Ambola ni rafiki yako sana”

“Ndiyo ni rafiki yangu.Tulikutana siku moja

katika sherehe Fulani tangu hapo tukawa marafiki.”alisema Salma

“Ninataka kufahamu mahali anakoishi.Unaweza ukanielekeza tafadhali? Aliuliza Mathew

“Unataka kumtembelea? Yule ni mchumba wa mtu sasa hivi” alisema Salma kwa utani wote wakaangua kicheko.

“Hapana kuna jambo ninataka kuzungumza naye la muhimu”alisema Mathew

“Huna namba yake ya simu? Aliuliza Salma

“Ninahitaji kuonana naye ana kwa ana lakini nitaomba pia unipe namba yake ya simu kama hutajali” alisema Mathew.Salma alimuelekeza nyumbani kwa Ambola halafu akampa namba ya simu anayotumia Ambola.Mathew alimshukuru wakaagana akarejea garini.

“Kuwa na mahusiano na watu mbali mbali inasaidia sana” alisema Mathew huku akimpatia Ruby karatasi yenye

namba ya simu ya Ambola aliyopewa na Salma.

"Namba hii ni tofauti na ile iliyopopo katika tovuti" alisema Ruby huku akiiandika katika simu yake akapiga.

*"Samahani namba ya simu unayopiga haipo.Tafadhali angalia namba kwa umakini kisha jaribu kupiga tena.Kwa msaada zaidi wasiliana na huduma kwa wateja"* ndivyo aliyvojibibiwa Ruby baada ya kupiga namba ile.Ruby

alichoka akashusha pumzi na kumtazama Mathew.

"Jibu ni lile lile kama la mwanzo namba hii haipatikani" alisema Ruby.Mathew aliichukua simu akampigia Salma.

"Ndiyo Mathew" alisema Salma

"Salma samahani kwa kukusumbua.Lini uliwasiliana na Ambola kwa kutumia namba hii uliyonipa? Aliuliza Mathew

"Siku tatu zilizopita."

“Ahsante sana” alijibu Mathew na kukata simu.

“Namba hii ilikuwa inatumika.Salma anadai aliwasiliana na Ambola juzi” alisema Mathew

“Nini kimetokea hadi isipatikane tena? Aliuliza Ruby

“Ni mapema kusema lakini inaonekana namba hii imekwisha ondolewa katika orodha ya namba za simu hapa nchini.”

“Kwa nini iondolewe katika orodha ya namba za simu?

“Lazima ipo sababu.Lakini tuendelee kwanza kufanya uchunguzi tutabaini kwa nini namba hii haipo” alisema Mathew

“Tunaelekea wapi sasa hivi? Aliuliza Ruby

“Kwa sasa tunaelekea nyumbani kwa Ambola” alisema Mathew

Walifuata maelekezo waliyopewa na Salma

wakajikuta wamefika nyumbani kwa Ambola.Walipatwa na mshangao mkubwa kwa kile walichokikuta mahali hapo.Gari la mizigo lilikuwa linashusha vitu vya ndani vikiingizwa katika nyumba hiyo.Ilimlazimu Mathew kushuka garini akaenda kusalimiana na kijana mmoja aliyekuwa amesimama pembeni akitoa maelekezo kwa vijana waliokuwa wanashusha mizigo.

“Karibu kaka” alisema yule jamaa halafu akamuacha

Mathew akaenda kutoa maelekezo kisha akarudi kwa Mathew

“Kaka karibu.Hawa vijana inabidi uwe nao karibu vinginevyo wanaweza wakaharibu vyombo.”

“Nimeshtuka baada ya kufika hapa na kukuta kuna shughuli inaendelea.Unahamia humu ndani? Aliuliza Mathew

“Ndiyo ninahamia”

“Aliyekuwa akiishi humu amehama?

“Hapana sifahamu.Mimi nyumba hii nimeinunua sifahamu awali nani alikuwa anakaa humu.Nililetwa hapa na dalali ambaye nilimpa kazi ya kunitafutia nyumba.”alisema yule jamaa

“Ninamdai fedha nyingi mtu aliyekuwa akiishi humu na yawezekana ameamua kuuza nyumba kimya kimya akakimbia.Unaweza ukanisaidia mawasiliano na huyo dalali tafadhali? Aliuliza Mathew.Yule jamaa ambaye alionekana kutohitaji maneno mengi alimpatia Mathew

namba ya simu ya dalali ambaye alimsaidia kupata ile nyumba wakaagana Mathew akaondoka akarejea garini.

“Mambo bado magumu” alisema Mathew akamueleza Ruby kile kilichotokea.Baada ya majadiliano mafupi Ruby akaipiga ile namba ya dalali.Simu ilipokelewa.

“Hallo habari yako kaka” alisema Ruby

“Tunamshukuru Mungu tunaendelea vizuri.” Alisema jamaa aliyepokea simu

“Samahani kaka nina shida na dalali Muddy.Ni wewe? Aliuliza Ruby

“Samahani dada yangu.Huyu dalali Muddy unamfahamu?

“Simfahamu ila nimepewa namba na mtu.Ninataka kuonana naye anisaidie kutafuta nyumba”

“Pole dada huyu dalali amefariki ghafla alfajiri ya leo”

“Amefariki? Aliuliza Ruby kwa mshangao.

“Ndiyo.Amefariki dunia alfajiri ya leo na tayari tumekwisha mzika.Hapa tupo msibani”

“Nini sababu ya kifo chake? Alikuwa mgonjwa? Ruby aliuliza

“Kwa mujibu wa mke wake, alianza kukohoa ilipofika saa tisa usiku.Ilipofika saa kumi na moja hali ilibadilika akashindwa kupumua.Walimbeba kumpeleka hospitali lakini

alifia njiani” alisema yule jamaa

“Ahsante kwa taarifa na poleni sana kwa msiba” alisema Ruby akakata simu.

Ruby alimpa Mathew taarifa ile ambayo ilizidi kuwachanganya.

“Mathew ninazidi kuingiwa na hofu kubwa.” Alisema Ruby

“Kuna swali moja ambalo tunahitaji kulitafutia jibu pia.Ambola ni nani? Aliuliza Mathew

“Kutoweka kwake ghafla kunazua maswali.Kwa nini namba yake haipo tena wakati juzi ilikuwa inapatikana? Nyuma yake imeuzwa kwa haraka sana na hajulikani alipo.Biashara yake pia imefungwa.Matukio haya yote yametokea katika kipindi kifupi sana.Swali linarudi lile lile Ambola ni nani? Aliuliza Mathew

“Mathew sifahamu wapi pa kupata majibu ya swali hilo.” Alisema Ruby

“Usihofu Ruby.Wakati wote mwanzo huwa mgumu sana.Kwa sasa tutafute namna ya kuonana na Gavana wa benki kuu ” alisema Mathew

NDUGU MSOMAJI,MATHEW MULUMBI AMEFIKA DAR ES SALAAM AMBAKO ANAKUTANA NA MAMBO YANAYOMFANYA AJIULIZE SWALI GUMU
*AMBOLA NI NANI?*
FUATANA NA SHUJAA MATHEW MULUMBI KATIKA MKASA HUU WA KUSISIMUA.